

SIKU YA USHINDI



Mwaweza kuketi mkipenda. Nami ninataka kutoa shukrani zangu kwa Mungu, kwa majaliwa ya kuwa hapa na kukutana na raia wenzangu wa Ufalme wa Mungu. Wakati ninyi watu mmekusanyika hapa, asubuhi ya leo, katika nyumba ya ndugu huyu, ku—kufanya ushirika pamoja, kwa namna fulani inanikumbusha juu ya Kanisa la mwanzoni. Jinsi Ukristo ulivyoanza hapo kwanza, ilikuwa, Biblia ilisema, “Ilikuwa ni nyumba kwa nyumba. Walikutana na kuumea mkate kwa moyo mmoja.” Na hilo ndilo tunalotaka kufanya asubuhi hii, wakati tukiwa hapa, ni umoja wa moyo, kusudi moja.

² Ja—jambo moja tunalojaribu kufanikisha, na, hilo ni, kuutimiza mpango wa Mungu kwa ajili ya maisha yetu, wakati tukiwa hapa duniani. Na labda, huenda ikawa, Mungu, maelfu mengi ya miaka iliyopita, lakini Yeye ni, kwa hekima Yake isiyo na kikomo, alijua ya kwamba tungekuwa hapa asubuhi ya leo, na tungekuwa huku nyuma kwenye mbuga hii pana, ama—ama jangwa hapa, kwenye jengo hili dogo. Alijua hilo maelfu ya miaka iliyopita.

³ Sasa, tulikutana na baadhi ya marafiki zetu waliokuwa wakija huku asubuhi ya leo kutoka Tucson, familia ya Stricker. Nao walikuwa wameharibikiwa na jenereta kwenye gari lao. Tuliwakusanya wale tulioweza, kuwaleta huku, mama huyu hapa na wa—watoto. Nao wanakuja, baadaye kidogo, endapo wanaweza kuitengeneza jenereta yao. Ilikuwa ni kwenye maskini njia panda hapa nje. Sijui ilikuwa ni wapi. Bali tuna furaha kuwa hapa.

⁴ Na sasa, Ndugu Isaacson hapa, na tunafahamiana kidogo sana, si zaidi ya vile tu tunajua ya kwamba sisi ni ndugu katika Kristo. Nasi tumekuwa na nyakati za ushirika pamoja. Nami naamini mkutano wetu wa kwanza ulikuwa kwenye... kule Phoenix, miaka mingi iliyopita. Na kama mke wake yupo, nisingemfahamu. Sasa, hivyo ndivyo vizuri tunavyofahamiana, kujua mke wake ni nani, ama familia yake.

⁵ Nikiingia nilikutana na mmoja wa ndugu zetu weusi amesimama mlangoni, jamaa mzuri sana mwenye kupeana mikono, mwajua, ikakufanya ujisikie kwamba umekaribishwa tu vizuri sana, wajua, kuingia, na—na kuwa miongoni mwa hawa wanaoonekana kama umati asubuhi ya leo, nalo linanipa majaliwa.

⁶ Na sasa, nimekuwa na fursa ya kuzungumza katika sehemu nyingi zilizojaa watu, ambako wangekuwa na labda maelfu mara maelfu ya watu wamekusanyika. Bali mimi... Kumbukumbu za huduma yangu ni nyakati kama hizi, wakati kuna labda dazani

moja, ama mbili, wameketi pamoja, inavyoonekana kwamba Mungu huwashughulikia watu kwa karibu zaidi. Nafikiri tunajisikia kufahamiana zaidi, na—na wakati tukikusanyika katika kusanyiko dogo. Inaonekana kama mahali ambapo Neno la Mungu ni—ni maarufu sana kwetu, ni wakati sisi, Yeye alisema, “Walipo wawili au watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nipo papo hapo miongoni mwao.”

⁷ Jana usiku, karibu na usiku wa manane, nilikuwa tu nimekutanika na...katika nyumba ambapo palikuwa na mwanamume na mke wake, na msichana mdogo, aliyekuwa anaingia kichaa, juu ya maskini tukio fulani lililokuwa limetukia. Na wakati tuna...tulipokuwa tumekusanyika pamoja, mimi tu na msichana huyo mdogo, katika chumba, maana mambo yaliyopaswa kusemwa, yalikuwa, ni afadhali tungekuwa pamoja. Ndipo basi ikatokea Nuru hii, Malaika huyu wa Bwana, naye akajumuika moja kwa moja mahali tulipokuwa, ikionyesha ya kwamba—ya kwamba Mungu hutimiza ahadi Yake.

⁸ Pia jana, ambapo kulikuwako na kijana mwanamume mwenye umri wa miaka ishirini na miwili, wa familia maarufu sana, alikuwa ameshikwa na matumbwitumbwi, nayo matumbwitumbwi yalikuwa yamemwangukia. Na wengi wenu watu wazima mnajua hiyo ni nini, hasa katika wanaume. Wanaume, kwa kweli karibu huwaua. Basi mvulana huyu, kwa siku kadhaa, majuma mawili mfululizo, alikuwa na homa ya nyuzi joto mia moja na tano. Sasa, mnajua hiyo ni hali ya kushikwa na kiharusi pale. Nao madaktari walikuwa wamejaribu yote waliyoweza, kwa penisilini na kila kitu, kuiondolea mbali hiyo homa kutokana na uambukizi huo. Lakini ilionekana kana kwamba haikusaidia lolote. Bali katika muda wa dakika moja mbele za Mungu, kila alama ya homa hiyo ilimwacha kijana mwanamume huyo. Akasimama, mzima. Basi inaonyesha tu Mtu muhimu ni Kristo.

⁹ Hilo ndilo kusudi la sisi kuwa hapa, asubuhi ya leo katika nyumba hii, ni kumtumikia Kristo, kwenye siku hii ya sabato.

¹⁰ Nimeutazamia wakati huu wa kuja huku, kukutana na ndugu yetu wa thamani, na nyinyi watu. Nimepokea zaka zenu ambazo ndugu amenitumia, mara nyingi, kutoka kwenye kusanyiko hili dogo hapa nje. Na hazina kama hizo, ninazishikilia kwa heshima sana kwa utu wangu mwenyewe, kwa sababu ninajua ya kwamba sina budi kuwajibika siku moja kwamba zilienda wapi kutoka hapo. Na hakika ninataka kushukuru, ninashukuru, na ninataka kutoa shukrani zangu kwa uaminifu wenu ninyi watu, kwa—kwa wazo hili ambalo mmetekeleza, mkijua ya kwamba zaka mlizo nazo. Na kukutana katika nyumba kama hizi na, hata hivyo, mnataka kidogo mlicheo nacho kiende, kwa yote mjuayo, katika kuisaidia hu—huduma. Basi, tangu hapo na kuendelea, sina budi kuwajibika kwa ajili

yake. Nami ninataka kuwa mkadamu mzuri kwa Bwana wetu, na wakati itanibidi kujibu kwenye Siku ile, kwa yale tumefanya duniani.

¹¹ Sasa, kuna jambo moja, huku nyuma hatusumbuliwi sana na mingurumo ya magari, na hilo ni zuri.

¹² Na kwa hiyo sasa, karibu sijui namna ya kusema jambo hili, bali laiti tungalikuwa tukifanya uamsho hapa nyuma, ambapo tuna siku kadhaa zake. Kwa sababu, kwa njia hii, unaingia tu na kusema, “Mu hali gani? Nina furaha kukutana nanyi,” na kuzungumza dakika chache kumhusu Bwana, kisha umeondoka tena. Ninapaswa kuwa Tucson saa saba u nusu. Na jinsi ambavyo hiyo... Tunakutana tu hapa namna hiyo, na kupeana mikono sisi kwa sisi, na kusema, “U hali gani? Nafurahi kukutana nawe,” kisha unaondoka.

¹³ Lakini, mwajua, ninawazia juu ya Siku moja wakati tutakutana ambapo hatutasema kwaheri. Hatutasema, “Ni vema kukuona. Natumaini utarudi tena.” Ambapo, tutahesabu hapa labda saa kadhaa pamoja. Huko tunaweza, huenda tukaketi chini na kuzungumza miaka milioni moja, kukiweco na kitu kama wakati, nasi hatuta—hakutakuwako na wakati mfupi zaidi kuliko vile ilivyokuwa tulipoketi chini. Mnaona? Ni Umilele tu. Hakuna—hakuna mwisho wake. Na kuwazia juu ya wakati ambapo tuko nje, na jinsi hiyo, na wakati tutakapotembea kupitia ushoroba wa paradiso kuu ya Mungu, huku Malaika wakiimba nyimbo rasmi.

¹⁴ Na—na sasa ndio wakati ambapo hatuna budi ku—kupiga vita, kushinda vita, na kuyashinda mambo ya ulimwengu.

¹⁵ Na Kule, vema, hakutakuwako na vita vyovyote Kule. Ombi la mwisho litafanywa; haitawabidi kufanya mikutano ya maombi tena. Hakutakuwako tena na mahali pa watu kuokoka. Hakutakuwako na ugonjwa wa kuponywa. Nalo litakuwa tu ni jambo moja kuu tukufu.

¹⁶ Basi kama binadamu, asubuhi ya leo, tu—tungeahidi nini? Tungeangalia nini ambacho kingekuwa ni kikuu kuliko kuiangalia ile ahadi ya wakati huo. Mnaona?

¹⁷ Tunawazia... hapa ninaangalia kwenye mabadiliko ya nyakati, kutoka kwenye watoto wachanga wa kunyonya juu ya mapaja ya mama zao, kufikia wavulana wadogo wa shuleni, wasichana matineja na wavulana, na halafu umri wa makamu, na halafu mzee. Mnaona? Na—na mvulana wa shule, mwaka jana alikuwa kwenye paja la mama yake, mtoto mchanga wa kunyonya. Mnaona? Naye tineja aliingia shuleni mwaka jana tu, inaonekana. Halafu mwenye umri wa makamu alikuwa umri wa tineja. Halafu umri wa uzeeni. Ninii tu... Loo! Mnaona? Ni kama tu mvuke unaoruka ukaingia duniani na kuanguka. Sulemani alisema, ninaamini ilikuwa, “Ni kama ua.

Linachipuka, kisha linakatwa, na kunyauka.” Basi tu—tunataka kunufaika kutokana na wakati tulio nao hapa.

¹⁸ Kwa hiyo sasa hebu tunene na Yeye, sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu katika maombi.

¹⁹ Na kama kungekuwako na mtu yeyote hapa ambaye angetaka kukumbukwa katika maombi, kwa mfano, kama kuwa mgonjwa, ama yuna haja, kama tu ungefanya lijulikane kwa Mungu moyoni mwako, useme, “Sasa, Bwana, nimeingia, ku—kuomba ombi hili.” Na kama ungeninii tu, ili kwamba ninjue, kwa namna fulani, kama tu ungeinua mkono wako juu, na kuninii tu, namna hiyo, useme, “Nikumbuke.” Bwana awabariki sana.

²⁰ Mwenyezi Mungu, uliyeziumba mbingu na nchi, kwa Neno Lako, tumekusanyika hapa asubuhi ya leo kuzungumza juu ya Neno hili, na juu ya Yule aliye mkuu Ambaye ni Neno.

²¹ Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya majaliwa haya makuu ya kurudi upande wa nyuma ya jangwa. Ilikuwa ni hapo siku moja ambapo kichaka kilichowaka moto kiliuvutia usikivu wa nabii mtoro. Ndipo hapo akaagizwa upya, kisha akatumwa, ambaye alifanyika mkombozi mkuu wa watu wa siku hiyo, wa urithi wa Mungu uliokuwa utumwani. Ee Mungu mkuu, si uje upande wa nyuma ya jangwa asubuhi ya leo pamoja nasi? Tujuavyo sisi, Wewe uko kwenye makanisa makubwa ya dayosisi, na kote ulimwenguni. Lakini tukijua kwamba Wewe ni Mungu asiye na kikomo, na hakuna mahali palipo padogo kupita kiasi, ama hakuna mahali, ama, haijalishi tumetawanyika vizuri vipi kote katika uso wa nchi, hata hivyo Wewe umeenea kila mahali, unaweza kuwa kila mahali nyakati zote. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hili.

²² Na katika kusanyiko hili asubuhi ya leo, tunakushukuru Wewe kwa ajili ya ndugu yetu na—na kundi lake dogo hapa, na kwa ujasiri wao na uaminifu kwenye Huduma ya Mungu duniani leo hii, nasi tunaomba baraka Zako juu yao. Pia naomba, mradi tu kuna moyo ulio na shauku kwa ajili ya Kristo, jalia daima kuwe na mjumbe mahali fulani kutoa, kuuleta Ujumbe kwa moyo huo wenye njaa.

²³ Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, kwa ajili ya haja za hao watu ambao wameinua mikono yao sasa hivi. Unajua kilichokuwa kikipigapiga chini ya mkono wao, karibu na moyo wao. Walikuwa na haja. Kama ni maradhi, Bwana (Wewe Ambaye ulimchukua Paul Sharrit ambaye ndio kwanza azungumziwe saa kadhaa tu zilizopita, wakati alipokuwa amelala kati ya mauti na uzima, akiwa na homa kali mno ambayo sayansi yote ya matibabu isingeweza kukomesha, na hata hivyo neno moja dogo la maombi lilikomesha hiyo homa mara moja; Wewe ni Yehova Mungu), onyesha ya kwamba umewakilishwa vizuri tu, na u halisi tu leo, hapa upande wa nyuma ya jangwa

hili, kama ulivyokuwa katika siku za Musa upande wa nyuma ya jangwa kule.

²⁴ Tunakushukuru Wewe, kwa sababu ninajua kwamba Wewe utayasikia maombi. Nasi tunakuja Kwako kwa unyenyekevu mwingi na uaminifu kabisa, tukijua ya kwamba ingekuwa ni kosa kukuomba mambo ambayo tunayawazia tu niani mwetu. Tunataka kuwa wenye bidii na hakika kabisa, kwamba lile tuombalo, hatuna budi kuliadini, na—na—na kujua ya kwamba ni mapenzi ya Mungu kutujalia hilo, maana tumelitatia hilo mioyoni mwetu, kwa yote tujuayo, Bwana.

²⁵ Kwa hiyo, ninaomba ya kwamba utamponya kila mgonjwa aliye hapa asubuhi ya leo. Okoa kila mmoja aliyepotea. Tujalie. Jalia jambo fulani lisemwe ama lifanywe leo hii, ambalo litawasababisha, katika mahali ambapo wameketi, ama kusimama kandokando ya kuta, ama popote pale, kusudi imani inayotia nanga ya Mungu itaingia mioyoni mwao na hilo litalitua, kabisa. Lijalie, Baba.

²⁶ Mbariki ndugu ambaye ameturuhusu kuichukua nyumba hii hapa kwa ajili ya ibada.

²⁷ Sasa nena nasi kupitia Neno Lako, kwa kuwa hiyo ndiyo sababu tupo hapa, Bwana. Tunapenda kufanya ushirika sisi kwa sisi, bali hata hivyo ni Wewe ndiwe tunayetaka, Bwana. Tunaweza kwenda nje chini ya miti mahali fulani na kuketi chini na kusemezana mmoja kwa mwingine. Lakini, hapa, tumekusanyika kupata kibali Kwako. Hivi hutakutana nasi sasa, Bwana? Tumekifungua kiti moyoni mwetu, ili Wewe upate enzi leo hii, ukanene nasi, na kutwambia kuhusu haja tulizo nazo, na upendo Wako ulioonyeshwa kwetu tunapouonyesha upendo wetu Kwako. Haya tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁸ Hapo, kama kuna mtu fulani huko nyuma, anayetaka kuketi chini, ninaona viti fulani hapa, kwamba mngeweza kukusanyika, na mkitaka kupata starehe zaidi.

²⁹ Sasa, nyakati hizi tunazoishi ni nyakati nzuri mno. Basi jana, nilipokuwa nikiwazia niseme nini leo, nikijua nimetazamia kuja huku chini, basi nitasema nini nitakaposhuka, mkutano huu mdogo wa maombi? Ndipo nikamwomba Bwana anisaidie. Na—nami nikachukua muhtasari kidogo juu ya Maandiko hapa, ambayo ningetaka kuyaelezea kwenu enyi watu asubuhi ya leo, wakati tuingojea baraka za Bwana.

³⁰ Nasi tunaomba sasa ya kwamba utaufungua moyo wako na kufahamu mbisho ulio mdogo mno, hafifu sana wa Kristo moyoni mwako. Kumbuka, wewe, iwapo wewe si mwaminio, wala kamwe hujampokea Kristo bado, hili litakuwa ndilo jambo muhimu zaidi lililowahi kutokea kwako, tutakusanyika katika nyumba hii asubuhi ya leo, ili kwamba wakati mbisho huo utakapokuja moyoni mwako, kama utaukubali, ni mlango wa Uzima. Kuukataa ni mauti. Na hiyo ndiyo sababu tupo hapa

asubuhi ya leo, kukuonyesha ya kwamba kuna mlango ulio wazi kwa ajili ya kila mwaminio anayeweza kuamini.

³¹ Sasa ninataka kusoma kutoka kwenye Kitabu cha Ufunuo wa Yesu Kristo, mlango wa 15. Ninataka kusoma sehemu, vifungu vinne vya kwanza vya mlango wa 15 wa Kitabu cha Ufunuo:

Kisha nikaona ishara nyingine katika mbingu, iliyo kubwa na ya ajabu; malaika saba walio na...mapigo saba ya mwisho; maana katika hayo ghadhabu ya Mungu imetimia.

Tena nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo iliyochangamana na moto, na wale wenye kushinda, watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake, na kwa alama yake, na kwa hesabu ya jina lake, walisimama juu ya hiyo bahari ya kioo, wenye...vinubi vya Mungu.

Nao wakaimba wimbo wa Musa, mtumwa wa Mungu, na wimbo wa Mwana-Kondoo, wikisema, Ni makuu na ya ajabu, matendo yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi; ni za haki, na za kweli, njia zako, Ee Mfalme wa watakatifu.

Ni nani asiyekucha, Ee Bwana, na kulitukuza jina lako? Kwa kuwa wewe peke yako u Mtakatifu; na mataifa yote watakuja na kusujudu mbele zako; kwa kuwa matendo yako ya haki yamekwisha kufunuliwa.

³² Basi Bwana akipenda, ningetaka kuchukua fungu kutoka kwenye hayo, kuliita siku ya Ushindi, *Siku Ya Ushindi*, tunapolifananisha hilo, ushindi mkamilifu.

³³ Hawa watu, ambao kwenye mlango ambao tunaninii... ndio kwanza tuusome, walikuwa ndio kwanza wapate ushindi. Nafikiri kwamba neno *ushindi* ni neno kuu katika lugha ya Kiingereza. Linamaanisha ya kwamba ume—umemshinda adui, na umeshinda, nawe ni mshindi anayeshikilia ushindi. Nasi huimba nyimbo na kushangilia katika ushindi. Basi hapa tunaona ya kwamba kulikuwako na jambo fulani, watu hawa walikuwa wamekuja kwenye bahari hii ya kioo, iliyochangamana na moto. Nao walikuwa wamepata ushindi juu ya yule mnyama, juu ya sanamu yake, juu ya alama yake, na hesabu ya jina lake. Mambo haya yote, walikuwa wamepata ushindi juu yao, nao walikuwa ni washindi waliosimama ng'ambo ya pili, juu ya bahari ya kioo iliyochangamana na moto, wakiimba nyimbo za sifa kwa Mwenyezi Mungu.

³⁴ Sasa, kuzungumza juu ya ushindi na siku za Ushindi, na kadhalika, inaturejesha kwenye wazo la vita, tunapowazia juu ya siku ya Ushindi. Kwa sababu, hivi karibuni tu, katika miaka michache iliyopita, tulifikia kwenye si—si—siku tunayoita siku ya Ushindi, ya vita hivyo, ambapo walipata ushindi juu ya adui. Na ni vibaya sana kwamba inatubidi kuiwazia, lakini

ulimwengu umeloweshwa na damu ya binadamu tangu ile damu ya Habili mwenye haki.

³⁵ Damu ya kwanza ya binadamu kuigusa nchi ilikuwa ni ya Habili mwenye haki. Naye, sababu ya yeye kuimwaga damu yake, ilikuwa ni kwa sababu alikuwa sahihi na Mungu. Naye Mungu alikuwa ameukubali u—upatanisho wake aliokuwa nao, kwa imani alikuwa amemtotea Mungu, mwana-kondoo huyu.

³⁶ Ndipo ndugu yake mwenye wivu, akimwonea wivu, akamwua Habili mwenye haki. Na sababu iyo hiyo imeninii, karibu tu, imesababisha kumwagwa kwa damu yote ya binadamu juu ya uso wa dunia. Na dunia ya kale hakika imeloweshwa kwayo, ya wote kote ulimwenguni, damu ya binadamu. Sisi... Kuna sababu yake. Kuna sababu ambayo wangukuwa, ya kumwagwa kwa damu hii ya binadamu. Na tunaona ya kwamba sababu ya kwanza ilikuwa ni kwa sababu ya wivu, kwamba—kwamba Kaini alimwonea Habili wivu kwa maana Mungu aliikubali dhabihu ya Habili. Nayo Waebrania 11 inatwambia ya kwamba—ya kwamba—ya kwamba, “Habili alimtotea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko ile ya Kaini, na Mungu akishuhudia kwayo.” Naye Kaini, bila shaka, akiwa na wivu juu ya hili, kwa sababu dhabihu yake ilikataliwa, na ya Habili kukubaliwa. Naye Habili alifanya hili kwa imani. Biblia ilisema ya kwamba alifanya hili “kwa imani.”

³⁷ Kuona kwamba—kwamba, hao wavulana wawili wakijaribu kupata kibali kwa Mungu, wapate kurudi, kwa sababu wanajua kwamba walikuwa wametoka tu kwenye bustani ya Uzima. Nao walikuwa wameanguka, upande ule mwingine, kwa makosa ya wazazi wao, yalikuwa yamewaweka katika hali ya kufa; kama tu sisi sote tunavyosimama, asubuhi ya leo, katika hali ya kufa. Nao walitaka kujua jinsi ya kurudi mahali hapo ambapo wangeweza kupata Uzima tena. Basi, katika kufanya hivyo, wa—walikuwa wakijaribu kupata kibali kwa Mungu.

³⁸ Ndipo Kaini akatoa dhabibu ya kupendeza ya maua na matunda ya kondeni, ama chochote kilichokuwa alichoweka juu ya yale madhabahu.

³⁹ Bali Habili, kwa ufunuo wa kiroho, ilifunuliwa kwake ya kwamba si matunda ya kondeni yaliyosababisha mauti. “Damu ndiyo iliyosababisha mauti.” Kwa hiyo, akatoa damu ya kibadala kisicho na hatia, na Mungu akaikubali. Na hiyo imekuwa ndiyo upatanisho wa Mungu kwa ajili ya dhambi zetu, tangu siku iyo hiyo. Hakuna njia nyingine, kwa sababu kama alikuwa ameikubali kwa msingi mwingine wowote, basi ingalitubidi kuja juu ya msingi huo, ili kuwa, kupata kibali cha Mungu. Lakini Mungu alikubali tu damu isiyo na hatia ya kitu kisicho na hatia. Mnaona?

⁴⁰ Hivyo basi, kama urembo na mahali pakubwa pangukuwa ndipo kibali cha Mungu, leo hii tungeninii... Tungeshangaa,

“Hivi Yeye angerudi upande wa nyuma ya jangwa, kwenye makazi haya madogo hapa karibu na njia ya reli? Hivi Yeye angerudi hapa na kukutana nasi?” Bali kama ingalikuwa ni kanisa kubwa la dayosisi, ama urembo ambao—ambao Kaini alitoa, mbona, tungekuta tumekuwa tu tukijizungumzia wenyewe, na hewani.

⁴¹ Bali Mungu alikuja juu ya msingi wa damu iliyomwagika. Kwa hiyo, haijalishi, leo hii, jinsi tulivyo wadogo, jinsi tulivyo maskini, ama jinsi ambavyo tungetaka kuwa, kumtolea Mungu mahali pakubwa zaidi, bali Mungu asingepakubali, si zaidi ya vile atapakubali sasa hivi, kwa sababu tunakuja juu ya msingi wa Damu iliyomwagika ya Kibadala kisicho na hatia, ambacho ni Kristo akifa kwa ajili yetu sisi wenye dhambi.

⁴² Sasa, sababu ya hii Damu kumwagwa, ni kwa sababu, ninaamini, ya kwamba mwanadamu anataka kuninii. . . Mungu anamwalika mwanadamu kutazama, bali mwanadamu anataka ku—kujionyesha mwenyewe. Mwanadamu anataka kutazama kile Mungu anachojaribu kumwonyesha, juu ya msingi wa wa—wazo lake mwenyewe kukihusu. Mnaona? Mungu anajaribu kumwonyesha mwanadamu kitu fulani, bali mwanadamu anataka kukikubali juu ya yale yeye. . . jinsi anavyokiona.

⁴³ Lakini ni kama tu mtu yeyote anayetaka kuonyesha tukio. Hapana budi pawe na sababu ya kuonyesha tukio hili. Kuna. . . Kama ukisema, “Tazama huko mlimani,” sasa kuna kitu fulani huko ambacho kilikuvutia, ambacho unajaribu kuniomba nitazame mlima huo. Unaona? Ama, “Tazama mti huu,” unaona, kuna jambo fulani kuuhusu mti huo ambalo unanitaka nione.

⁴⁴ Sasa, Mungu anajaribu kumfanya mtu akitazame kile Kibadala kisicho na hatia kwa ajili ya njia ya kurudi. Naye mwanadamu anataka kukitazama kwa njia yake mwenyewe. Hataki kuona kile Mungu anachojaribu kumwonyesha, katika Kibadala hiki kisicho na hatia. Kwa hiyo, hiyo ndiyo iliyosababisha matatizo. Halafu, mtu anapofanya hivyo, tuseme, anachukua darubini, kutazama mbali, kuona kile Mungu anachojaribu kumwonyesha, yeye hushindwa kurekebisha darubini yake vizuri.

⁴⁵ Hapa barabarani, si muda mrefu uliopita, tukija kutoka kwenye ziara ya huko juu milimani, mtu fulani alisema, “Hapa, chukua darubini hii na uangalie *hapa* kwenye kitu fulani.” Vema, niliichukua hiyo darubini. Nikaona vitu vitatu au vinne mbalimbali. Sasa, mnaona, nilijua ya kwamba kulikuwa na kasoro fulani na hiyo. Mnaona? Sasa, paa huyu aliyesimama kondeni, ilionekana kama wako watatu ama wanne wamesimama pamoja. Sasa, jambo ni kwamba, huyo paa alikuwa ni paa mmoja kikamilifu. Darubini ilikuwa sawa. Lakini niliyopaswa kufanya, ilikuwa ni kurekebisha hiyo fokasi mpaka niwafanye hao paa watatu kuwa mmoja, na

kumfanya paa mmoja. Mnaona? Halafu basi kwamba... Mnaona, nyuma yangu, nilijua kulikuwako na...kuwa ni paa mmoja, kwa sababu hivyo ndivyo nilivyoambiwa. Lakini kuichukua hiyo darubini na kutazama, niliona, tuseme, paa watatu wamesimama pale. Vema, hiyo darubini ilikuwa haikurekebisha vizuri kwenye lengo. Si—sina budi kuirekebisha darubini hiyo kwenye lengo, mpaka niifikishe mahali ambapo ninaona paa mmoja. Halafu basi darubini inamvuta kwangu karibu vya kutosha hata ninaweza kuona sura yake ilivyo.

⁴⁶ Sasa, Mungu hutupa Biblia. Sasa, Biblia ni Neno, nalo Neno ni Mungu. Kwa hiyo, hilo ndilo darubini yetu. Hilo ndilo miwani yetu. Lakini, basi, tunapoanza kuangalia katika Biblia, na kuona njia nne ama tano mbalimbali, vema, inahitaji kurekebisha kwenye lengo, mnaona. Na sisi—sisi inatubidi kulenga kitu hicho kufikia mahali ambapo tunaweza kuona kusudi moja taadhimu la Mungu.

⁴⁷ Bali mwanadamu anataka kuunda dhehebu, akimbilie *huku*. Naye huyo mwingine anataka kuninii, “Vema, sininii... Nafikiri ninaweza kuwa jamaa mkubwa kuliko yeye, kwa hiyo nitaanzia *hapa*. Tutawafunza wavulana wetu vizuri zaidi, na tutafanya *hivi* na kadhalika.” Mnaona? Wanashindwa kurekebisha darubini kwenye lengo. Mungu anawataka waone jambo moja, na hilo ni Damu isiyo na hatia iliyomwagwa kwa ajili ya dhambi zao. Hilo ndilo hasa. Hilo ndilo jambo halisi, haidhuru. Hatuhitaji dhehebu. Sina kitu dhidi yao, ila tu wao... madhara wanayofanya, kuwavuta watu na kutenganisha udugu na kadhalika.

⁴⁸ Lakini tunapaswa tu kutazama kitu kimoja, na hicho ni Kibadala chetu. Hiyo ni kweli. Na Kibadala hicho ni Yesu Kristo.

⁴⁹ Halafu basi leo hii mnaona jinsi tumepotoshwa katika madhehebu. Nao wanasema, “Wamethodisti wana uamsho. Hakika, hilo halimaanishi Wabaptisti. Hao ni Wamethodisti. Na *hawa* wana uamsho, na kadhalika.” Na wao—wao wanamkatilia mbali jamaa huyo mwingine, wakati wote. Lakini hatutaki kuliona namna hiyo.

⁵⁰ Tunataka kuendelea kurekebisha hilo lengo mpaka tuone kwamba kuna Mungu mmoja. Unapoona wakiwa watatu huko nje, afadhali urekebishe darubini kwenye lengo vizuri zaidi. Unaona? Una—unaona kitu vibaya. Kwa hiyo afadhali uingize ndani, na uone kuna Mungu mmoja juu yetu sote, na Yeye ndiye Mungu wa jamii ya binadamu.

⁵¹ Na kama Yeye ni Mungu, kwa vyovyote, anajali kila mwanadamu, kwa sababu ni kiumbe Chake. Naye anawajali watoto. Anajali umri wa uzeeni na umri wa makamu. Anajali ra—rangi zetu, na weupe, wa hudhurungi, weusi, wa—wa manjano, namna mbalimbali za ngozi zetu kutokana na nchi

tulimotoka na babu yetu. Yeye anatumia sisi sote. Hawajali tu Wayahudi, pekee, ama ja—ama jamii ya kimanjano, jamii ya watu weusi, jamii ya wazungu, yoyote ile.

⁵² Anajali jamii yote ya binadamu, na anajaribu kuifanya jamii yote ya binadamu kulenga Neno Lake mpaka kufikia jambo moja, na kusema, “Kuna Mungu mmoja, na Mungu huyo alitoa Kibadala kisicho na hatia, kwa kuja; kufanyika, Mwenyewe, Mwanadamu, kusudi aiondoe dhambi, kuiokoa jamii nzima ya binadamu.” Nabii Yohana alieleza vizuri sana, “Tazama Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu,” yeyote yule. Tatizo lote la dhambi limetatuliwa papo hapo katika Kibadala hicho kimoja kisicho na hatia.

⁵³ Lakini wakati mtu anapoanza kuchukua darubini ya Mungu hapa, a—anaanza kuninii. . . Yeye anaangalia mengi sana ya kawaida, anashindwa kuona matumizi ya kiroho ambayo Neno hutoa.

⁵⁴ Sasa, mnaona, hilo ndilo moja la mambo makuu ambayo mtu hufanya wakati akijaribu kutazama, kwa sababu yeye hutazama kama Kaini alivyotazama kwa darubini. Yeye alitazama u—ufanisi wa kibinafsi. Kaini aliwazia, “Sasa, kama ninaweza kumwondoa Habili njiani, basi mimi ndimi peke yangu. Ndipo, mnaona, hapo, huyo jamaa mwingine ameondolewa.” Hivyo ndivyo mwanadamu amejaribu kufanya, kote katika miaka, ni kujaribu kumwondoa jamaa huyo mwingine njiani.

⁵⁵ Wakati, anapaswa kuwa akijaribu kumleta jamaa huyo mwingine njiani pamoja naye, na—na awe ndugu, mnaona, badala ya kujaribu kusema, “Loo, kundi hilo dogo, wafagilie tu mbali. Na hili *hapa*, loo, vema, wako *hivi*, ama *vile*.” Mnaona? Hatupaswi kufanya hivyo. Tunapaswa kuwa tukijaribu kuleta kitu hicho chote kwenye picha mo—moja nzima, na hiyo ni Yesu Kristo.

⁵⁶ Msichana mmoja, jana usiku, kwenye mahojiano, yeye alisema. . . Lakini alisema. . . Binti ya mhudumu alikuwa amekuwa na namna fulani ya uhusiano mdogo wa kimapenzi, na—naye alikuwa amerukwa na akili juu yake. Alienda, alichanganyikiwa. Msichana mrembo sana, na yapata umri wa miaka ishirini na mitatu.

⁵⁷ Na alipokuwa msichana mdogo, mwenye umri wa kama miaka kumi na miwili, alikuwa huko Chicago. Na akiwa ameketi mkutanoni. . . Ama, Elgin, ndiko ilikuwa. Basi akiketi mkutanoni, Roho Mtakatifu alipitia kwenye kusanyiko na kumwita, kwamba alikuwa ni nani, na kusema, “Una moyo unaonong’ona. Daktari anasema huwezi kuishi ukafikia umri wa miaka kumi na mitano. Lakini, BWANA ASEMA HIVI, umeponywa.” Naye kamwe hata—kamwe hata hakuhihi ugonjwa wa moyo, tangu.

⁵⁸ Basi jana usiku alikuwa na aina tofauti ya ugonjwa wa moyo. Ulikuwa ni ugonjwa wa kiroho, wa moyo. Mpenzi wake alikuwa ametoroka na kumwoa mwanamke mwingine. Na, hata hivyo, alikuwa angali anampenda. Naye mvulana huyu akimwambia kwamba anampenda, bado, anampenda, na “baba yake alikuwa ameisababisha.”

⁵⁹ Nikasema, “Loo, upuuzi. Haikumlazimu kumwoa msichana huyo mwingine. Alifanya hivyo kwa sababu alishindwa kuwa na namna nzuri ya upendo kwako.” Hiyo ni kweli kabisa.

⁶⁰ Lakini, mnaona, akiwa amechanganyikiwa kabisa katika hilo, msichana huyo aliketi hapo a—amejitweza sana, ilivyoonekana. Naye akasema, “Loo, ninajua Johnny ananipenda. Ninajua.” Mnaona? Hilo tu ndilo angaliweza kuona. Aliishi katika ulimwengu huo mmoja mdogo, peke yake, aliokuwa amejiingiza mle ndani.

⁶¹ Basi nikaushika mkono wake. Nikasema, “Nisikilize mimi.” Ndipo Bwana akaonyesha ono, mnaona, ambalo alijua sikujua chochote kulihusu, kwamba jambo fulani lilikuwa limetukia, shughuli fulani kati yao. Basi hilo liliposemwa, ndipo hilo likamzindua upesi sana. Nikasema, “Sasa, wakati ukiwa umetoka huko, tazama Kalvari. Hapo, unatoka hapa nje na kuanza kunywa pombe, nawe ni binti wa mhudumu, binti wa mhudumu wa Kipentekoste, na kufanya mambo unayofanya, ukijaribu kufifisha huzuni hiyo; mtu huyo, na mtu ambaye hakujali wewe hata kwa mwaliko wa kidole.” Nikasema. “Tazama huko Kalvari, ewe msichana. Hiyo ndiyo njia pekee ya kurudi.”

⁶² Inatupasa kujiweka kwenye lengo, hata, tuishi au tufe, tudidimie ama tuzame, ni Kalvari, Kristo. Hicho ndicho kitu ambacho Mungu anatumia tukirejee.

⁶³ Nao watu, wakiwa wamelilenga Neno la Mungu, badala ya kulileta pamoja na kulifanya liseme jambo moja ambalo Mungu analifanya kusema, tunaangalia upande wa kawaida. Hivyo basi, li—linaninii, mtu anayefanya hivyo, anajifikisha mahali ambapo anafuatilia tu kitu kilichowasilishwa. “Hii hapa fursa ambayo sisi, sisi kundi dogo, tunaweza kufanya *hili*, na tunaweza. . . Hatutakuwa na uhusiano wowote na hao wengine.” Basi—basi hilo, mnaona, hilo ndilo jambo la kwanza lililowasilishwa; badala ya kulenga ndani, kujua ya kwamba ni upendano wa ndugu ndio tunaopaswa kuwa nao mmoja kwa mwingine, na—na kuelewana mmoja kwa mwingine, na kupendana mmoja kwa mwingine, na kuabudu pamoja mmoja na mwingine. Wanashusha mtu hadhi kwa sababu ya nguo anazovaa, ama ninii—ama elimu aliyo nayo, ama rangi ya ngozi yake, ama—ama kitu kama hicho. Ama ninii yake. . . Na hilo, kwa hiyo, linawatenganisha watu, naye mtu analifuata hilo.

⁶⁴ Kamwe haimpi mtu wa ndani nafasi ya kufanya kazi. Sasa, sisi ni—sisi ni viumbe wa utatu: nafsi, mwili, na roho. Sasa, lakini wakati nia ya kawaida... Zile nguvu mbili za kiroho zinazotenda kazi ndani yako ni nia yako na ninii yako—na roho yako. Unaona? Sasa, nia ya kimaumbile, ambayo imestaarabika sana, itajaribu kufanikisha jambo fulani kwa akili yake. Unaona? Ndipo wakati anapofanya hivyo, jambo lile lile anapofanya hivyo, anajitenga mwenyewe mbali na mtu wa kiroho aliye ndani yake. Na hapo ndipo matatizo yanapotokea, papo hapo, mnaona, anajaribu kulifanikisha mwenyewe.

⁶⁵ Kama nilivyonena hapa, sio muda mrefu uliopita, ninaamini ilikuwa kwenye maskani, ya kwamba, “Mungu ni mkuu sana, Yeye anaweza kuwa rahisi sana.”

⁶⁶ Sasa, mnaona, tunapokuwa wakuu, hatuwezi kuwa rahisi. Mnaona? Sisi, tunajua mengi kupita kiasi. Na sisi—sisi hatuna budi kuninii, “Loo, haina budi kuwa jinsi *hii* tu, jinsi tunavyolisema, la sivyo Hilo haliko hivyo, hata kidogo.” Mnaona? Vema, kwa njia hiyo, tunamkosa Mungu.

⁶⁷ Lakini kama mtu angalininii tu, mtu mashuhuri, angezidi kuwa tu mkubwa zaidi na zaidi, na kuendelea kuwa mkubwa, yeye angefanya nini? Angerudi tu moja kwa moja kuwa tena mnyenyekevu sana, na rahisi sana, mpaka watu wanatembea juu yake bila kujua, mnaona, mtu mashuhuri aliye miongoni mwao.

⁶⁸ Ni jambo lile lile tu kama tunalofanya. Tu—tunapima elektroni, tunaipasua atomu, na tunatuma u—ujumbe mwezini, kisha tunatembea juu ya nyasi za kawaida tusizojua lolote kuzihusu. Hiyo ni kweli. Maskini ua dogo, hakuna mtu anayeweza kulielezea au anayeweza kupata uhai unaojificha kwenye mbegu hiyo ndogo iliyo chini ardhini, itakayochipusha ua mwaka ujao. Kijani cha kawaida cha nyasi, wanasayansi wote ulimwenguni wasingeweza kufanya kichipuko kimoja cha nyasi, hata kijani kimoja. Mnaona? Huwezi kukifanya, kwa sababu kinashikilia uhai. Na kwa hiyo, mnaona, sisi... .

⁶⁹ Imesemwa, “Wapumbavu hutembea na viatu vya njumu ambako Malaika wanaogopa kukanyaga.” Na hilo ni kweli kabisa. Tunatembea juu ya mambo rahisi. Tunatembea juu ya Mungu.

⁷⁰ Tunatembea juu ya—ya orchidi, tukitafuta daisi. Sasa, ndiyo hiyo, mnaona, kutembea juu ya orchidi. Laiti tungejifanya tu rahisi, tushuke. Hakuna mtu angaliangalia hata kwenye ninii... .

⁷¹ Ule mzabibu pale nje, ni kitu gani? Mungu. Ni kitu gani? Ni majivu ya volkano, yenye uhai ndani yake. Geukeni, angalieni huko, kuna mti mkubwa mno unaosimama pale, mti wa pamba, ninaamini. Ni kitu gani? Ni majivu ya volkano, yenye uhai tofauti ndani yake. Uhai wa namna *hii*, ulifanya—uliufanya mti. Uhai wa namna *ile*, ulifanya mzabibu. Mnaona?

⁷² Na sisi ni kitu gani? Majivu ya volkano, yenye uhai ndani yake. Ni kitu gani kilichotufanya kile tulicho? Tungekuwa tu si zaidi ya hicho, bali Mungu aliweka Uzima wa Milele ndani yetu, ndipo basi tunakuwa raia wa Mungu. Halafu, tuna—tunaangalia, tunalenga Neno kujirekebisha basi kwa Mungu.

⁷³ Bali mwanadamu kamwe hampi mtu wa ndani nafasi ya kuelezea yaliyo sahihi, kwa hiyo hilo ndilo linalosababisha matatizo. Angalieni. Tunaona, asipofanya hivyo, basi kunafanyika nini? Tunaona ya kwamba hasira yake, kama Kaini, ilipanda, mnaona, upesi sana. Alishikwa na wivu. Hakutaka Mungu, atoe ninii yake, aikubali ninii ya Kaini... Dhabihu ya Habili badala ya yake. Alitaka kwenda, pia. Alitaka dhabihu yake mwenyewe. Alitaka njia yake mwenyewe, mnaona, badala ya kumjia Habili, na kusema, “Loo, ndugu yangu, nina furaha sana ya kwamba Mungu amekubali. Sasa tunayo njia, ambapo tunajua ya kwamba Yehova anaikubali njia hii, kwa sababu ameithibitisha kwa kuipokea dhabihu yako.” Hilo si lingekuwa ndilo jambo la—la kufanya? Lakini badala ya hilo, alishikwa na wivu.

⁷⁴ Sasa, hivi hamwoni jambo lilo hilo leo hii katika watu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaona? Ni njia yake tu, mnaona, sasa, badala ya kukubali njia ambayo Mungu anathibitisha kwamba ni Kweli.

⁷⁵ Njia ambayo Mungu Mwenyewe hujitokeza jukwaani, na kusema, “*Hii* ndiyo. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona Mimi tena; hata hivyo ninyi mtaniona Mimi, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu.” Mnaona, ulimwengu, ninyi... “Ulimwengu hautaniona Mimi, bali ninyi mtaniona.” Mnaona, “Kaini hataniona Mimi, bali wewe utaniona, Habili.” Mnaona? Kwa sababu, ni—ni jambo lile lile.

⁷⁶ Basi badala ya kuja na kusema, “Vema, ajabu sana, tunamwona Mungu miongoni mwa watu, akitenda kazi, hebu tufanye hivyo,” la, bwana, kwa kanuni za imani, jambo lile lile, na, tamaa, hasa, na pamoja na wivu, kitu kile kile alichu nacho Kaini, anahitaji damu ya ndugu yake. Yeye anajaribu kumfagilia mbali aondoke njiani, kumwondolea mbali. “Hao si kitu ila kundi la watakatifu wanaojibingirisha. Ni wadogo.” Mnaona? Mnajua ninalomaanisha. Hilo ndilo linaloanzisha matatizo. Hapo ndipo matatizo huanzia. Hapo ndipo nadhiri zilizovunjwa. Hapo ndipo ushirika uliovunjika unapotenganishwa. Hicho ndicho kitu kinachozivunjia mbali nyumba. Hilo ndilo jambo linalofanya gu—gurudumu lianze kusonga kuelekea kwenye talaka. Hilo ndilo jambo lenyewe linalovunja ushirika.

⁷⁷ Hilo ndilo jambo lililovunja ushirika kule Edeni, ni kwa sababu kwamba Hawa alishindwa kushikilia lile lengo, ya

kuangalia kwake Neno la Mungu, na akasikiliza hoja za adui. Mnaona? Mnaona? Laiti angedumu tu moja kwa moja na, “Mungu alisema hivyo. Hilo latosha. Mungu alisema hivyo,” bali hakutaka kufanya hivyo. Mnaona? Yeye alibadilisha lengo la darubini yake, akaanza kuona, badala ya kuwapo tu na njia moja, zikawa njia mbili. Mnaona? Yeye aliona, “Vema, sasa, labda mtu huyu anaweza kuwa sahihi. Labda yuko sahihi. Sasa, tunajua Mungu yu sahihi, na labda yu sahihi. Hii ni nuru tu zaidi juu ya yale Mungu aliyosema.” Mnaona hapo?

⁷⁸ Hilo hapo jambo lile lile linatukia leo hii, moja kwa moja kurejea mahali pale pale. Mnaona? Mnaona? Unaona mawazo mawili. Kunalo moja tu. Kabisa hakuna kanuni ya imani. Ni Neno, ni Neno la Mungu, kusudi la Mungu, mpango wa Mungu. Mipango mingine yote haifai kitu.

⁷⁹ Hilo, basi Hawa alifanya jambo hili ovu, na hiyo ndiyo sababu leo hii kwamba Mungu, katika Neno Lake, kamwe hawaruhusu wanawake kuwa wahudumu. Mnaona? Kamwe haliruhusiwi katika Neno.

⁸⁰ Asubuhi ya leo, nyumbani kwetu, tulikuwa tukizungumza, huku tumeketi kwenye meza ya kiamshakinywa, mapema. Tulikuwa tukitaka kuanza, ili tupate kufika hapa kwa wakati mzuri, kisha turudi kwenye miadi hiyo nyingine. Kwa hiyo, sisi, nikasema... Tulikuwa tukizungumza mezani. Na—nasi tulikuwa tukizungumza juu ya ninii, neno likaibuka, kuhusu Malaika. Mvulana wangu mdogo, Joseph, anayeketi pale, alisema jambo fulani juu ya Malaika. Naye akasema, “Sasa, baba,” akasema, “Malaika...”

Nikasema, “Mungu ni Mwanamume.”

“Lakini,” kasema, “Ma—Malaika ni wanawake.”

Nikasema, “Hakuna kitu kama hicho.” Mnaona? Akasema...

⁸¹ “Vema, Wao wananinii...” Sarah, binti yangu, kasema, “Lakini, baba,” kasema, “pale, wao, wanavaa sketi.” Kasema, “Hao, hao ni wanawake.”

Nikasema, “Hiyo ni, mwanasaikolojia fulani aliichora picha hiyo.”

⁸² Kamwe hawakuona, katika Biblia, Malaika akiitwa “mwanamke.” Ilikuwa ni “mwanamume,” sikuzote, mwanamume, mwanamume, mwanamume, si—si “mwanamke.” Hakuna kitu kama Malaika kuwa mwanamke. Kamwe hakujawahi kuwapo, katika Biblia. Wala hakuna, katika Kanisa la Mungu aliye hai. Hakuna kitu kama mjumbe mwanamke. *Malaika* ni “mjumbe.” Kwa hiyo, Mungu kamwe haliruhusu.

⁸³ Kwa sababu, Biblia inasema, “Adamu aliumbwa kwanza, na Hawa baadaye. Wala Adamu hakudanganywa, bali mwanamke kwa kudanganywa aliingia katika hali ya kukosa.” Mnaona? Kwa

hiyo, yeye. . . Kasema, Paulo alisema, “Simruhusu mwanamke kufundisha, wala kuwa na mamlaka, bali kuwa katika utulivu, kama pia i—isemavyo torati.”

⁸⁴ Sasa, katika jambo hilo, mnaona, sasa, sasa, kama vile makundi yetu ya Kipentekoste, ndiyo kiini cha hilo. Mnaona? Wanachofanya, wanaweka fokasi, “Vema, sasa, hapa, huyu hapa mwanamke anayeweza kuhubiri kama radi.” Vema, hilo halina shaka, hata kidogo. Kweli kabisa. Niliwasikia wahubiri fulani wanawake, wangeweza kuhubiri, ambapo wanaume wasingeweza kusimama hata kwenye kivuli cha kufanya hilo, bali hilo halina uhusiano wowote na yaliyo haki; mnaona, halina hata mmoja.

⁸⁵ Paulo alisema, “Kama mtu akinena kwa lugha na pasiwepo na mfasiri, basi na anyamaze.”

Wasema, “Siwezi kunyamaza.”

⁸⁶ Lakini Biblia ilisema unaweza, unaona, kwa hiyo jambo ndilo hilo. Mnaona? Halina budi kufanywa kwa utaratibu, kuwekwa katika utaratibu, kuwekwa mahali pake, na hapo daima libaki mahali pake.

⁸⁷ Mnaona, hapo, unapoteza lengo. Hilo linasababisha chuki, uroho, na kadhalika. Badala ya kujirekebisha wenyewe kujirejesha kwenye Neno, tunajirekebisha wenyewe nje ya lengo, na kuona, “Vema, acha wafanye waonacho.” Mnaona, namna hiyo, hivyo tu, basi. Vema.

⁸⁸ Sasa, tunaona ya kwamba inavunja ushirika wa nyumba. Inavunja ushirika wa makanisa. Inavunja ushirika wa mataifa, jambo lile lile.

⁸⁹ Mataifa yanataka kuona njia yao yenyewe. Ujerumani inataka kuona njia yao, pekee. Urusi inataka kuona njia yao, pekee. Marekani inataka kuona njia yake, pekee. Mnaona? Halafu, mnaona, jambo ndilo hilo. Ni roho ya mataifa. Unaikuta popote uendapo, unakuta roho ya kitaifa. Niliingia, nao wana njia mbalimbali. Ni la kigeni sana. Kama ningalikuwa na wakati, ningetaka tu kurukaruka kupitia baadhi ya mataifa na kuwaonyesha.

⁹⁰ Unapoingia ndani, ukiingia Ujerumani, unakuta roho ya kijeshi. Kila kitu ni kijeshi. Inakubidi kusimama wima, utembe sawasawa, upige kona zako, na kila kitu. Ni kijeshi.

⁹¹ Ukiingia Ufaransa, unakuta roho ya utovu wa uadilifu: wanawake tu, na mvinyo, na pombe, na—na upuuzi kama huo. Mnaona?

⁹² Ukiingia Ufini, unapata roho ya utiifu, kwa namna fulani, kila kitu ni kiaminifu. “Hatuna budi kulipia kila kitu.” Mnaona? Halina budi kutimizwa. Inabidi tu iwe hivyo. Haidhuru itawabidi kufanya kazi kwa nguvu jinsi gani, gharama yake, haina budi kuwa hivyo.

⁹³ Ukija Marekani, unakuta, “Ha, ha, ha, ha, ha!” kubwa. Hivyo ndivyo ilivyo. Naam. Hiyo ndiyo roho ya Marekani. Mtu fulani anatoa mzaha mchafu kwenye redio, na kila mtu anaucheka. Ernie Ford, ama—ama baadhi yao, wakifanya mizaha waliyo nayo, mwajua, kila mahali, Arthur Godfrey na kundi hilo namna hiyo, mnaona, hiyo ni—hiyo ndiyo roho ya Marekani. Unaikuta hivyo.

⁹⁴ Halafu roho hizo zinaona wivu moja kwa nyingine. Nazo zinafanya nini? Zinasababisha vita. Hiyo ni kweli.

⁹⁵ Sasa, unaona, kila taifa linatawaliwa na Shetani. Biblia ilisema hivyo. Yeye ndiye mungu wa mataifa. Shetani alimpandisha Yesu juu, kwenye kilele cha mlima, kisha kasema... akamwonyesha falme zote zilizokuwa ulimwenguni, falme zote, katika dakika moja. Kasema, “Hizi ni zangu. Ninafanya nazo lolote nitakalo kufanya.” Kasema, “Nitakupua Wewe, kama utaniabudu.”

⁹⁶ Yesu akasema, “Rudi nyuma Yangu, Shetani.” Alijua atazirithi katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Mnaona? Kwa hiyo, haikumbidi kumsujudia. Alijua zitakuwa...

⁹⁷ Sasa, Mungu atakapokuja tena, na kuchukua, kufanya Ufalme Wake hapa, mnaona, hakutakuwapo na roho zozote za aina mbalimbali: roho ya Kijerumani, na roho ya Kifaransa, na ro—roho ya Kinorwe, na roho ya Kimarekani. Hakutakuwako na hizo. Itakuwa ni Roho mmoja, amina, Roho wa Mungu, akiishi katika kila moyo. Hiyo ni kweli. Na kutakuwako na bendera moja, taifa moja, watu wamoja, udugu, Ubaba wa Mungu, na udugu wa binadamu. Uwana! Naam.

⁹⁸ Kisha tunaona ya kwamba, kwa sababu kwamba watu hufanya jambo hili, na—na kusababisha mizozo hii mikubwa, na kadhalika... Sasa, mnaona, mradi tu Shetani anautawala, kutakuwako na vita na matatizo, na vita. Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu... Mathayo Mtakatifu 24, kasema, “Mtasikia habari za vita, na tetesi za vita, na vita, na vita.” Kwa nini? Maana, mtawala wa dunia, Shetani, nguvu za mataifa... Kuna roho ya kitaifa *hapa*, roho ya kitaifa *hapa*. Ni pepo. Hayawezi kuelewana mmoja na mwingine. Mnaona?

⁹⁹ Uliwahi kuchukua kundi katika nchi ya Eskimo kule juu, ambako tunabebwa na magari ya kukokotwa ya mbwa, Alaska kaskazini, na huko juu kabisa karibu na Himaya ya Kaskazini magharibi? Wakati ki—kiongozi pale alipokuwa akiwafunga hawa mbwa, walioitwa Huskies... Basi alimfunga mmoja *hapa*, na mmoja *pale*, na mmoja *hapa*.

Nikasema, “Unafanya hivyo kwa sababu gani?”

¹⁰⁰ Akasema, “Wamejawa sana na ibilisi, wangeuana wao kwa wao.” Mnaona? Ku—kuua tu, hilo tu ndilo wanalofikiria.

¹⁰¹ Vema, huyo—huyo ni ibilisi, mnaona. Yeye ni mwuaji. Yeye, yeye tu, ta—taifa linaninii tu... Hata ibilisi wakipigana na ibilisi. Mnaona? Wanashambuliana tu wao kwa wao.

Lakini, Mungu ni upendo mtupu, mnaona, kwa hiyo hamwezi kufanya lolote ila kupendana ninyi kwa ninyi.

¹⁰² Kwa hiyo, mnaona, kanuni yote inalenga kurejea moja kwa moja tena kwenye hizo roho, kurudi moja kwa moja kwenye mwanzo. Mwanzo ndio mlango wa mbegu, nao huzaa kila kitu, basi, tulicho nacho duniani leo hii.

¹⁰³ Sasa tunavyo vita na ushindi, ushindi mkuu. Taifa moja litaingia na kulipiga hilo lingine, liseme, “Utukufu! Tumepata ushindi. Tuliwapiga.” Na—na halafu, muda si muda mwajua, watakuwa marafiki na kupeana mikono, na kufanya biashara kati yao.

¹⁰⁴ Kisha baada ya kitambo kidogo, ni rais mwingine, ama mfalme mwingine ataingia, ama mtawala mwingine, mfumo mwingine. Basi, muda si muda mwajua, hawa hapa, wajukuu wao wamerudi na bunduki, wakipigana wao kwa wao, tena. “Vita, na tetesi za vita.” Ndipo huyu mwingine atamshambulia huyo mwingine, “Sasa mtanitumikia, mwajua. Mimi ndimi mshindi, nawe ni—wewe ndiye uliye nje.” Na kadhalika. Unaninii tu...

¹⁰⁵ Kama vile nilivyosikia tamshi fulani wakati mmoja, “Mungu alimfanya mwanadamu, naye mwanadamu akawafanya watumwa.” Mungu hakumfanya mtu apate kumtawala mwingine. Mungu alimfanya mwanadamu wapate kuwa ni ndugu, hiyo ni kweli, kuwa ndugu, sio mmoja kumtawala mwingine. Hakuna jamii iliyo bora zaidi, hakuna taifa lililo kuu, hakuna lugha bora zaidi. Tuna lugha moja, ya Kimbinguni. Mnaona? Hiyo ni kweli. Tuna udugu mmoja: huo ni wa mwanadamu. Huo ni wa mwanadamu, haidhuru yeye ni nani.

¹⁰⁶ Kwa nini tupigane na kuuana? Lakini wanafanya hivyo. Ndipo wakati mwingine, taifa zuri, ama taifa lililo na mfumo ndani yake, linajaribu kufanya yaliyo haki, na kupigania haki zake, ndipo taifa ovu litaingia liwe juu yake. Halafu basi hapa watachukua mamlaka, nalo taifa *hili* litakuwa *lile*. Kisha huku na huku, kubadilika tu, huku na huku.

¹⁰⁷ Mataifa yamekuwa na ushindi mwingi, mwingi sana wa kitaifa ambao wamejaribu, wakati wamejaribu kupigania uhuru wao, na yale wanayoshikilia kama ya—yao. Nayo yana—yana nini? Mradi tu Shetani anayatawala, yataendelea kupigana. Bali yamepata ushindi mwingi mkuu, ushindi mkuu. Tungeweza kurudi nyuma, tangu mwanzo kabisa, na kuonyesha ambapo taifa limetawala taifa, na kusherehekea ushindi mkuu, na kadhalika.

¹⁰⁸ Kama vile, katika Vita vya Kwanza vya Dunia, wakati tulipokuwa na Vita vya Kwanza vya Dunia, wakati mengi ya mataifa yalipokusanyika na kukutana nchini Ujerumani. Na ambapo Wabelgiji na mataifa mbalimbali yalipokuwa yakipigana chini ya bendera mbalimbali, viliitwa Vita vya Kwanza vya Dunia. Sasa mimi. . .

¹⁰⁹ Kunao ndugu wawili walioketi hapa, ama watatu, labda wanne wenu, wanaoweza kukumbuka hilo. Ninaweza kuvikumbuka. Mimi nina hamsini na minne.

¹¹⁰ Nami nakumbuka, kama mvulana mdogo, yapata umri wa miaka tisa, miaka minane ama tisa, mwaka wa 1914. Hebu tuone, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne. Nilikuwa na umri wa miaka mitano wakati vilipoanza. Ninakumbuka wakati waliposema kutakuwako na vita. Naye baba yangu alikuwa na kama ishirini na miwili, nao iliwabidi kumpeleka vitani. Loo, nisingeliwazia hilo, kumpeleka baba yangu vitani. Alipanda barabarani. Alikuwa kwenye mkokoteni wa springi. Naye alikuwa na. . . Naye alikuwa ameshuka kwenda ghalani, ambalo lilikuwa maili kadhaa chini yetu, naye alikuwa na gunia la maharagwe mle. Sisi. . . Na kwa hiyo nikasema. . . Nikachukua hayo maharagwe. Nikawaza, “Kama hao wakija na kuanzisha vita vyovyote, nitawapiga kwa gunia hili la maharagwe wakija.” Mnaona? Sasa, walikuwa ninii. . . Wazo tu la vita, ikimbidi baba yangu kwenda vitani!

¹¹¹ Vema, pa—parapanda ikalia, na—na ile “Nunueni hati zenu,” na kadhalika.

¹¹² Na kama sisi sote tunavyokumbuka, “Tutaenda kule na kupigana Vita hivi vya Dunia, nasi tutapata suluhu. Ndipo watafanya utaratibu.” Waliunda kile walichokiita Shirikisho la Mataifa. “Na ndipo kutakuwako na amani, amani ya Milele. Hivyo tu. Hakuna vita tena.”

¹¹³ Katika takriban miaka ishirini, tulikuwa tumevirudia moja kwa moja tena, vimewaka moto kadiri vilivyopata kuwaka, katika vita vingine vya dunia. Mnaona? Vita! Kwa nini? Ni tamaa, wivu. Mnaona? Mara Kaiser Wilhelm alipoondoka Ujerumani, basi jamaa mwingine akaingia, jina lake Adolf Hitler, Muaustria, naye akazivuruga kabisa akili za watu hao, ambalo limevuviwa na ibilisi, kwamba wangeweza kuupiga ulimwengu mzima. Ndipo, hao, na haya basi. Mnaona? Ni ibilisi dhidi ya ibilisi, tena, mnaona, namna hiyo. Nao raia wasio na hatia wa mataifa hayo, ambapo, hao huongozana tu vitani, vitani, vitani. Na imekuwa tu hivyo, sikuzote.

¹¹⁴ Sasa, sasa, tunaona, basi, jambo lingine mwajua, vita vingine vikaibuka. Sasa, tena, ulimwengu mzima ukaingia vitani tena, ukiwa na zana bora zaidi, na ndege bora zaidi, na mabomu makubwa zaidi. Nao wakapigana, na kutokwa na damu, na kufa,

na kufa kwa njaa, na kuganda, na kila kitu kingine. Vita, vita, vita!

¹¹⁵ Ndipo ikaja siku, tunayoita, siku ya Ushindi. Hapo ndipo nilipotoa somo hili, hiyo siku ya Ushindi, Siku ya Ushindi. Hiyo ni siku waliyopata ushindi, na ambako ma—majeshi yalipopata ushindi juu ya majeshi mengine, siku ya Ushindi. Sasa, kulikuwako na siku Mashuhuri, halafu kulikuwako na siku ya Ushindi. Siku Mashuhuri ni wakati walipoenda kupigana. Siku ya Ushindi ndipo amani ilipotiwa sahihi, wakati Ujerumani na mataifa mengine waliyoungana nayo na wote walijisalimisha kwa—kwa—mataifa mengine.

¹¹⁶ Nasi tulifanya nini? Kwenye siku ya Ushindi, tuliimba nyimbo. Tukapiga mayowe. Tukazitupa kofia zetu hewani. Tulitupa risasi hewani kwa bunduki. Tulilia. Tukapiga filimbi. Tukapiga ngoma. Tukaninii, tukacheza muziki. Tukaninii, tukapapasana mgongoni. Ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni ushindi. Loo, tulipata ushindi. Jinsi ambavyo hizi... Mbona, tulijisikia, “Tumeshinda. Tumeshinda.” Bendera zikapandishwa juu, nazo baragumu zikalia, na, loo, ni wakati wa jinsi gani tuliokuwa nao! “Ushindi, ushindi, ushindi! Tulishinda.”

¹¹⁷ Na lilikuwa ni jambo kuu. Lilileta amani kwa—kwa mataifa ya Kikristo, yanavyojiita. Ndipo tukawa na wakati mfupi wa kupumua. Baadhi ya wavulana waliokuwa hai, wakarudi nyumbani na kadhalika. Lakini, siku nyingi kuu, hizo, zimekuwako, nyingi za hizo, na vita vikuu.

¹¹⁸ Lakini, mnajua, kila mara ambapo kumekuwako na vita vya aina hiyo vilivyopiganwa, kumekuwako pia na watu wanaomwamini Mungu wamekuwa na siku nyingi kuu za Ushindi, pia. Loo, naam! Wamekuwako pande zote mbili, ambapo darubini zimeelekezwa na zikaenda upande wa kimaumbile, pamoja na siku za Ushindi; pia mahali linaporekebishwa kulenga ndani ya Neno katika Maandiko, linaleta siku nyingine ya Ushindi wakati mwingine.

¹¹⁹ Tumekuwa na vingi vya vita hivyo vikuu dhidi ya adui yetu. Naye Mungu amekuwa na watu mashuhuri hapa nje ambao wamesimama mbele, ambao wameweza ku—kuteka, kwa Roho wa Mungu, mawazo ya watu, na kuyaingiza katika Ufalme wa Mungu huko ng'ambo, na kuibuka washindi.

¹²⁰ Tunalipiga vita kila siku. Kila Mkristo hupiga vita, kila siku. Tuko kwenye vita sasa hivi, vinavyoendelea siku zote ndani yetu, kati ya mema na mabaya. “Tutalipokea? Tufanye nini? Tutasalimu amri kwa ulimwengu? Tutaliacha wazo hili tulilo nalo?”

¹²¹ Na kama tukilionga, tuliweke fokasi. Tulichukue kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Ni BWANA ASEMA HIVI, kila wakati, moja kwa moja kupitia pale. Hatuwezi kuliacha. Hatuwezi kupatana na hao wengine. Hatuwezi kabisa kufanya hivyo.

Inatubidi kukaa hapa. Hivyo tu. Haijalishi adui ni mkubwa jinsi gani, na ana mitambo kiasi gani dhidi yetu, na ni madhehebu mangapi, na ni mangapi ya *hili*, *lile*, ama *linginelo*. Sisi, hata hivyo, tumevuta fokasi hii, ya Neno la Mungu, mpaka tunakuta kwamba kuna kitu kimoja, na hicho ni Damu ya Yesu Kristo. Na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

¹²² Kwa hiyo, haileti tofauti yoyote yale asemayo mtu mwingine yeyote. Wao wanasema, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Hakuna ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, huo ulikuwa ni kwa ajili ya mitume peke yao.” Na mambo haya yote, wanajaribu kulenga mbali nalo. Hata hivyo, linarejesha kulenga moja kwa moja kwenye Neno, na hakuna mtu anayeweza kusema halipo. Hiyo ni kweli.

¹²³ Kwa hiyo, tuko katika vita. Na mashujaa wa Mungu daima wamekuwa na vita.

¹²⁴ Nanyi, kanisa dogo, kumbukeni hapa nyuma, ninyi ni sehemu ya umoja huo. Ninyi ni kituo cha mbali hapa nyuma. Kwamba, mnajua kituo cha mbali ni nini. Inawapasa, kwa kuwa baadhi yake papa hapa karibu nanyi. Kwa hiyo, ninyi ni kituo cha mbali hapa nyuma, kwenye mahali, ku—kushikilia bendera juu, kufanya yaliyo mema, kuendelea kudai Yesu Kristo ndiye tumaini pekee la ulimwengu; sio kanisa la Methodisti, kanisa la Baptisti, wazo la Kipresbiteri, Katoliki, ama Kiyahudi, ama chochote kiwezacho kuwa; jamii, ukoo, wala rangi. Hilo silo. Ni Yesu Kristo. Mnaona? Yeye Ndiye. Yeye ndiye Mshindi wetu. Yeye Ndiye. Yeye ndiye Jemadari Mkuu wa mwenendo huu. Hizi ndizo amri Zake. Hatuna budi kutekeleza amri. Ungewezaje kamwe. . .

¹²⁵ Baadhi yenu wavulana mlitumika katika vita. Mngewezaje kamwe. . . Jemadari atoe amri, nawe ugeuke na kufanya jambo lingine kinyumenyume, mbona, utalivuruga jeshi zima. Hiyo ni kweli. Utalitupa katika fujo. Huna budi kutekeleza amri. Jinsi tu unavyoweza kufanya hivyo, ni kulielekeza kwenye lengo, na kuona kusudi lake, kwamba inahusu nini. Vema.

¹²⁶ Tumekuwa na vita vingi vikuu, vita vya kiroho. Siku nyingi za Ushindi ambazo Kanisa limekuwa nazo; ninamaanisha Kanisa, Mwili wa Kristo. Sizungumzi juu ya mfumo wa dhehebu sasa. Ninazungumza juu ya Mwili wa Kristo. Mwili wa waaminio, kote katika nyakati, umekuwa na Siku nyingi kuu za ushindi.

¹²⁷ Tunazungumza kuhusu, tumekuwa na vita vingi, vita na tetesi za vita, na siku za Ushindi, na siku za Ushindi, na siku za Ushindi. Na hatimye zitaishia kwenye vita vikuu vya Har-Magedoni. Huo utakuwa ndio mwisho wake. Wakati litakapofikia kwenye vita vya Har-Magedoni, hivyo vitalitamaliza jambo hilo lote. Kabla tu ya ule Utawala mkuu

wa Miaka Elfu, Har-Magedoni vitaitakasa dunia. Itajitakasa tena kwa mlipuko huu wa atomiki, nayo majivu ya volkano na kadhalika yataizamisha damu hii ya wanadamu iliyolowa juu ya nchi, na dhambi na uhalifu. Inazama chini ya ardhi, nayo volkano inalipuka tena, na kufanya upya na kuitakasa nchi kwa ajili ya ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu. Yeye analisafisha Kanisa Lake, kwenye wakati huo, kwa ajili ya watu kuishi hapa. Amina. Na—nasema, napenda hilo. Naam, bwana. Wakati unakuja ambapo itakuwa zuri sana.

¹²⁸ Sasa, siku kuu za Ushindi, tunautafakari wakati huo. Hebu turudi nyuma tu. Tuna dakika chache sasa kuwazia juu ya baadhi ya hao mashujaa. Hebu turudi nyuma na kuwazia juu ya mmoja wa ninii. . . Tungeweza kurudi nyuma kabisa. Bali hebu turudi nyuma mbali tu kufikia Musa. Musa alikuwa na wakati ambapo alishuka katika vita vikuu, kwa sababu kanisa, lenyewe, lilikuwa limesahau ushindi kwa muda mrefu.

¹²⁹ Hiyo ndiyo shida ya kanisa leo hii. Kwa muda mrefu tumesahau ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tumesahau ya kwamba Mungu ni Mponya, anaweza kuwapa wagonjwa afya. Tulisahau ya kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ulimwagwa juu ya wanafunzi, na ukatolewa kutoka kizazi hadi kizazi, kwa mtu yeyote, yeyote atakaye angeweza kuja. Tumesahau hilo, muda mrefu, mrefu sana uliopita.

¹³⁰ Hivyo na Israeli ilikuwa imesahau. Walikuwa wameridhika huko chini Misri, kisha wakawa watumwa.

¹³¹ Na sasa huyu hapa alikuwa Musa aliyeshuka, katika mambo yake mwenyewe ya kiakili, ama, ufanisi wa kiakili kujaribu, na chini ya nguvu za kijeshi, kuwatoa Israeli, naye akashindwa kufanya hivyo.

¹³² Lakini Neno moja tu kutoka kwa Mungu, upande wa nyuma ya jangwa, lilichemsha kitu hicho chote tena. Ni kitu gani kilichompata Musa? Aliweka darubini yake sawasawa. Kusudi la Mungu la pekee halikuwa tu ni kumwoa msichana huyu mweusi mrembo wa Kushi kule nyuma, na—na kutulia na kupata watoto, na—na kuwachunga kondoo wa baba mkwe wake. Lakini utume wake ulikuwa—ulikuwa ni kuwakomboa wana wa Mungu, kutoka chini ya utumwa. Hilo lilikuwa ndilo agizo lake. Hilo ndilo kusudi la kuzaliwa kwake.

¹³³ Na kila mmoja wetu amezaliwa kwa ajili ya jambo fulani. Hatukuwekwa tu hapa bure. Mlima ule kamwe haukutokea huko nje kusudi tu uwe. Mti huo uliwekwa hapo kwa kusudi fulani. Kila kitu ni kwa kusudi fulani. Hakina budi kulitumikia. Nasi tuko hapa kwa kusudi fulani. Labda ni kumshuhudia mtu mmoja na kuwafanya waoko, na kutokana na huyo huenda akatokea mhubiri atakayepeleka nafsi milioni moja kwa Kristo.

¹³⁴ Hebu tazameni wongofu wa Dwight Moody, na wengi wa hao. Mnaona? Maskini mwanamke mmoja tu mkongwe, mwenye

ninii...Maskini mwanamke mkongwe mfua nguo akiwa na ujumbe moyoni mwake, kumfanyia Mungu jambo fulani, naye akakodi banda la kale la farasi, kisha akamleta mhubiri ashuke akahubiri. Na hakuna mtu ila maskini mvulana mdogo, mwenye nywele zilizoning'inia shingoni mwake, amevaa ukanda wa suruali ya baba yake, akashuka kule na kupiga magoti madhabahuni usiku huo. Dwight Moody, ambaye alipeleka nafsi nusu milioni kwa Yesu Kristo. Mnaona? Mwanamke huyo alikuwa na jambo la kufanya. Yeye ni...Ilikuwa ni kwa kusudi fulani. Alifanywa mwanamke mfua nguo, kwa kusudi fulani.

¹³⁵ Usidharau mahali Mungu amekuweka. Lakini, tumikia kusudi lako. Kunakuja siku kuu ya ushindi, moja ya siku hizi, ambapo vita vimekwisha.

¹³⁶ Sasa, angalia. Musa, alishuka, baada ya kuiweka darubini yake fokasi na kuona kwamba ilikuwa ni mpango wa Mungu, yale aliyopaswa kufanya. Akashuka. Akapiga vita vikali. Alikuwa na vita vingi vikuu. Lakini moja ya vita vyake vikuu, vya majaribu, ningetaka ku—kuvileta. Wakati, alipokuwa amefanikisha, kwa kuonyesha ishara na maajabu, kwa mambo mbalimbali ambayo Mungu alikuwa amemwonyesha, kunena Neno nalo lingeonekana na kutukia.

¹³⁷ Jambo lile lile tulilo nalo leo hii, kunena Neno juu ya wagonjwa, [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] na kuliona likiponya, na kufanya mambo haya mengine ambayo Neno la Mungu liliyanena kupitia midomo ya binadamu. “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usitie shaka, bali uamini yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.” Yesu alisema hivyo. Sasa, tunaamini hilo, na kulishikilia, na kulichukua, na kuliadini.

¹³⁸ Na sasa, Musa alikuwa amefanya hilo. Naye akashuka akaenda huko chini, naye Mungu alikuwa amethibitisha kuwa pamoja naye. Lakini baada ya kumshika kwa jumla, Mungu...

¹³⁹ Inaonekana kana kwamba, maisha ya Mkristo, ikiwa jamaa huyo hajajiweka kikamilifu ndani ya Kristo, maisha ya Kikristo, inaonekana, yanabeba masikitiko mengi sana. Bali masikitiko hayo ni—ni mapenzi ya Kiungu ya Mungu yakifanyika kwa ajili yetu. Sasa, haionekani kana kwamba ingekuwa ni hivyo, bali ni njia ya Mungu ya kufanya mambo. Yeye hutuacha tufikie mtoni, aone yale tutakayofanya.

¹⁴⁰ Musa aliwaongoza wana wa Israeli moja kwa moja kwenye njia ya wajibu wao, nalo jeshi la Farao likiwa nyuma yake, huku vumbi likichemka kutoka kwa watu nu—nusu milioni wenye silaha. Na hawa hapa Wayahudi milioni mbili wasiojiweza bila chochote, wamesimama pale, wanaume, wanawake, watoto, na kadhalika. Nayo Bahari ya Shamu ilikuwa imemzuia. Bahari ya chumvi ilikuwa imemzuia. Yeye...Hakuna mahali pa

kwenda. Mnaona? Bali Musa alikuwa na siku ya Ushindi wakati alipoomba kwa ushindi. Alienda akaanza kumlilia Bwana.

¹⁴¹ Ndipo Bwana akasema, “Mbona unanililia? Nilikuagiza kufanya hivyo. Nena na hao watoto, kwamba waendeleo kwenye wajibu wao.” Amina. Haya basi. “Usinililie. Umeagizwa kuwapeleka watu hawa huko. Nena nao tu, kwamba wasonge mbele, wakae moja kwa moja kwenye wajibu wao.” Amina.

¹⁴² Ni ujasiri wa jinsi gani huo unapaswa kuwa kwa mtu mgonjwa! Ni ujasiri wa jinsi gani huo unapaswa kuwa kwa mtu aliyerudi nyuma! Jigeuze mwenyewe urejee, uanze kurudi. Kaa kwenye wajibu. Ni kazi ya Mungu kuzifungua Bahari za Shamu. Ni kazi ya Mungu. Wewe nena tu na usonge mbele. Hayo ndiyo pekee yakupasayo kufanya.

¹⁴³ Naye Musa, ile siku kuu ya Ushindi, alikuwa baharini kule chini. Loo, ilikuwa ni siku ya Ushindi ya jinsi gani kwa Musa, na kwa wana wa Israeli ambao waliitii sauti ya nabii wao, wakati waliponena na kusonga mbele. Musa alisema, “Hivi mimi sija . . . Mmekwisha ona miujiza kumi tayari, na bado mnatilia shaka.” Ndipo akaanza kutembea kuelekea baharini, akiwa na ile fimbo mkononi mwake. Ndipo Mungu akatuma upepo usiku kucha na kuipulizia bahari hiyo kutoka upande mmoja hadi mwingine, nao wakavuka juu ya nchi kavu, siku ya Ushindi.

¹⁴⁴ Angalieni hapa. Wao walisimama, hata somo letu leo hii lilisema, kwamba, “Walisimama wakaimba wimbo wa Musa, kwenye bahari ya kioo iliyochangamana na moto.” Mnaona? Mnaona? Waliimba. Naye Musa, wakati alipovuka, naye hakujua la kufanya. Ndipo akavuka . . . Hili hapa jeshi la Farao linakuja, likijaribu kuiga mambo aliyokuwa akifanya. Kujilinganisha kimwili! Basi ilikuwaje? Bahari ilirudi ikawazamisha, kila mmoja. Naye akawaona wanyapara waliokufa.

¹⁴⁵ Miriamu akanyakua tari na huyo akashuka ufukoni, akipiga hii tari. Nao binti za Israeli wakamfuata, wikipiga makelele, na kupiga tari, na kucheza. Naye Musa akaimba katika Roho. Kama huo si mkutano wa mtindo wa kale wa Roho Mtakatifu, sijapata kuona mmoja. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁴⁶ “Hawa Wamisri mnaowatazama leo hii, hamtawaona tena.” Amina. Ni siku ya jinsi gani! Yote yamekwisha.

¹⁴⁷ Siku moja itakuja siku nyingine ya Ushindi kwa ajili ya Mkristo, pia. Hiyo ni kweli.

¹⁴⁸ Angalieni, Yoshua alikuwa na siku ya Ushindi huko mtoni, pia. Yoshua alikuwa na siku ya Ushindi huko Yeriko. Hakika alikuwa nayo. Pale ambapo alikuwa amevukia, alikuwa na siku ya Ushindi, kwanza, mtoni. Yule pale kwenye mwezi wa Aprili, labda maili moja ng'ambo ya pili, ndivyo Yordani ilivyokuwa, maana juu kwenye kilele cha milima huko juu, kuna theluji inayoyeyuka. Na kote kwenye nyanda, mto ulikuwa umesambaa.

¹⁴⁹ Basi hapana shaka huenda adui angalisema, “Sasa, Mungu ni Je—Jemadari kwelikweli, sivyo? Analiongoza jeshi lake moja kwa moja hapa juu wakati wa majani kuchipua, wakati mto uko kwenye hali yake mbaya zaidi, ambapo ndio wakati mbaya sana kuvuka, na halafu Yeye analiongoza jeshi lake hapa juu, na kuwaongoza wavuke.” La.

¹⁵⁰ Mungu huachilia masikitiko yatokee, apate kuonyesha ushindi. Loo, laiti tungaliweza tu kuona jambo hilo! Mnaona? Ungeona tu ya kwamba mambo haya yanayoonekana ya kukuchoma sana, na kukufadhaisha, hayo ni majaribu. Hayo ni mambo, kusimama kimya, kurekebisha darubini yako juu ya Neno la Mungu. Na kunena Neno, na kisha usonge tu mbele. Hayo ndiyo yote yaliyoko kufanya.

¹⁵¹ Tunafikia wakati, tunasema, “Mungu, sijui la kufanya. Nimekabibiliana nalo.”

¹⁵² Nena neno, “Bwana, ninaamini.” Kisha uanze tu kusonga mbele. Mungu huifungua bahari. Wewe unaendelea tu kutembea. Unaona?

¹⁵³ Sasa, tunaona ya kwamba Yoshua, moja kwa moja kwenye wakati huo, yeye aliomba. Ndipo Mungu akamwambia yale ambayo yangetendeka. Basi akawa na siku ya Ushindi. Alishinda. Halafu, wakati alipoushinda mto na akavuka ng’ambo ya pili, alifanya nini? Aliliweka lile sanduku. . .

¹⁵⁴ Ambalo, Neno lilikuwa ndani ya lile sanduku. Aliliweka hilo kwanza. Halafu waimbaji, na kadhalika, wakafuata nyuma yake. Lakini sanduku lilitangulia, kwanza.

¹⁵⁵ Wakati Israeli walipoenda vitani, kitu cha kwanza kilichotangulia kilikuwa ni waimbaji. Nao waimbaji wakaenda mbele, wakiimba. Ndipo wakapiga baragumu, na kadhalika. Ndipo sanduku likapanda juu. Halafu, wakati sanduku lilipopanda juu, basi wakaliweka hilo sanduku chini, ndipo vi—vita vikaanza.

¹⁵⁶ Angalieni. Lakini sasa, katika jambo hili, wakati Yoshua alipolichukua Neno kwanza, na kuliweka Neno kwanza, yeye alivuka ninii. . .

¹⁵⁷ Mungu alikuwa amemwambia, “Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja nawe. Sitakupungukia. Nitakuwa pamoja nawe. Hakuna mtu atakayesimama mbele zako, siku zote za maisha yako. Nitakuwa moja kwa moja pale. Usiogope yatakayotukia. Nitakuwa papo hapo.” Basi nini, akiwa na agizo kama hilo, Yoshua angefanya nini ila kuliweka Neno kwanza? Amina. Haya basi. Akiwa na agizo kutoka kwa Mungu, kuliweka Neno kwanza. Nalo likaleta siku ya Ushindi. Loo, halina budi kuja. Hivyo tu.

158 Aliliweka Neno kwanza, basi kulifanyika nini? Sanduku lilishuka kwanza, kwenye maji. Lilipofanya hivyo, bahari ikafunguka, ule mto, hasa, nao wakavuka.

159 Basi atafanya nini akifika kule? Ni jambo gani lingine litakalotukia, wakati atakapofika kule ng'ambo ya pili? Ndipo anakuta kwamba, wote wamezingirwa kwa ukuta, kwa sababu ya hofu juu yake wakati akija.

160 Lakini alikutana na Jemadari Mkuu, siku moja. Naye akawa na siku nyingine ya Ushindi. Alimwambia yale hasa ya kufanya, ndipo kuta za Yeriko zikapomoka. Anaenda kuifanya namna gani?

161 Mtu wa kimaumbile akiangalia kupitia darubini pale, atasema, "Sasa, hapa, Wewe ulinileta hapa, nami huyu hapa. Angalia upinzani. Mbona, wote wako ndani, wakiwa na makombeo yao. Kama tukiwahi kukaribia ukuta huo, ole wetu. Wanayo mawe yamewekwa mle, makombeo yao makubwa. Wana mikuki. Wana nyuta. Wana kila kitu kimewekwa mle. Nao wananinii tu. . ."

Lakini, mnaona, Yoshua alimweka Mungu kwanza. Naye alipofanya hivyo. . .

162 Si vile utakavyofika kule. Hilo ni juu ya Mungu. Endelea tu kusonga mbele, lifuate Neno.

163 Yeye akasema, "Uzungukeni, siku saba. Na kwenye siku ya saba, mzunguke mara saba. Kwenye. . . Kwenye mzunguko wa mwisho, pigeni baragumu." Mahali pa Mungu, kuondolea mbali mambo ya kawaida. Basi ya kiroho yakaingia, nazo hizo kuta zikapomoka. Nao wakapanda juu moja kwa moja na kuchukua kitu hicho. Naam, bwana. Mungu alikuwa na siku ya Ushindi wakati huo.

164 Ibrahimu alikuwa na siku ya Ushindi, baada ya kuahidiwa huyu mwana muda mrefu sana, Mungu akimjaribu kwa ajili ya upendo na uaminifu wake; ambaye sisi ni uzao wake, kama tunamwamini Mungu.

165 Naye Ibrahimu alikuwa na siku ya Ushindi. Ilikuwa lini? Ile siku alipoondoka nchi ya nyanda za Shinari? Sio hasa. Yeye alivuka, hiyo ni kweli, Efrati, akaja ng'ambo hii ya pili, kuwa mgeni. Hiyo ilikuwa ni siku nzuri. Hiyo bado ilikuwa kwa namna fulani. . .

166 Lakini siku yake kuu ya Ushindi ilikuwa juu ya Mlima Yire, wakati alipopanda kule juu siku hiyo, wakati Mungu alipompa jaribio la mwisho. Wakati, alikuwa na mwanawe wa pekee. Alisema, "Sasa, Ibrahimu, mpandishe kule juu kwenye mlima ule, na umtoe sadaka. Nimekufanya baba wa mataifa. Hiki hapa kitu pekee ulicho nacho, kukufanya 'baba wa mataifa,' ni kupitia kwa mtoto huyu. Ninataka umwue." Loo, mnalionga? "Angamiza kila kitu. Angamiza kusudi lenyewe. Wewe hapa, Ibrahimu, una

umri wa kama miaka mia moja na kumi na minne, kumi na mitano sasa. Nawe ulimngojea mtoto huyu kwa muda wa miaka ishirini na mitano. Na sasa mvulana huyu ana umri wa miaka kumi na mitano ama kumi na sita. Nami ninataka umchukue na kumwua, ili niweze kukufanya baba wa mataifa.” Loo, jamani! Naam.

¹⁶⁷ Ibrahimu kamwe hakutikisika. Kamwe, kamwe hakutetemeka kwa Neno la Mungu. Kasema, “Naam, Bwana. Mimi hapa ninaenda.” Akachukua kuni, akamchukua Isaka moja kwa moja kwenye kilele cha kilima, kwa utii hasa. Kwa nini? Aliweka amri ya Mungu kwanza. Atakuwaje Baba wa mataifa, wakati akiwa tu na mwana mmoja, na zaidi ya umri wa miaka mia moja sasa? Yeye alifanyaje hilo? Kwa sababu, hii, yeye alisema, “Mimi. . .” Yeye aliona ya kwamba kama Mungu aliweza kumpa Isaka, kama mmoja kutoka kwa wafu, angeweza pia kumfufua kutoka kwa wafu tena.

¹⁶⁸ Sasa, enyi marafiki, Mungu ambaye ametuinua kutoka kwenye mambo ya ulimwengu na upotovu wa dunia hii, hivi Yeye si anaweza hata na zaidi sana kutupa Uzima wa Milele na kutuweka katika Nchi ambamo hamna mauti? Mnaona? Tunaangalia majaribu haya madogo, na kufikiria ya kwamba hayo ni kitu. Mbona, hayo si kitu ila nyakati ndogondogo za kujaribiwa. Mnaona? Mungu alimjaribu Ibrahimu, lakini wakati alipopata siku yake ya Ushindi ni wakati alipopanda kule juu katika utii wa Neno.

¹⁶⁹ Kama wasemavyo siku hizi, “Ninajua.” Nilimsikia mhudumu muda mfupi uliopita, akisoma Matendo 2:38, bali alikosea, mnaona. Alisema, “Naye Petro alisema ya kwamba lazima wabatizwe, na kisha—kisha wangempokea Roho Mtakatifu,” akashindwa kusoma hayo mengine. Kwa nini? Mnaona, madhehebu yalishambulia Jambo lilo hilo. Sasa, mnalipata hilo wazo? Mnaona? Kwa nini mnafanya hivyo? Ni kitu gani kinachowafanya kuyakwepa Mambo hayo?

¹⁷⁰ Kama Biblia inasema Hilo, wewe lisome moja kwa moja jinsi inavyolisema, na useme jambo lile lile inalosema Biblia. Hapo ndipo unaporudisha fokasi yako vizuri, unaona, unarudi kwenye yale Neno liliyosema.

¹⁷¹ Sasa, tunaona ya kwamba, wao, unapata ninii ya—yako. . . unakosa fokasi pale.

¹⁷² Sasa, Ibrahimu alikuwa amerekebisha fokasi yake vizuri, kwa sababu Mungu alisema, “Nitakufanya baba wa mataifa,” wakati alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, naye Sara sitini na mitano.

¹⁷³ Naye akamwamini Mungu. Yeye, yeye alifanya nini? Aliweka fokasi yake juu ya kile BWANA ASEMA HIVI kilichokuwa. Naam, bwana. Naye akatembea moja kwa moja pamoja na hilo, kile BWANA ASEMA HIVI kilichokuwa. Siku baada ya

siku, alitembea. Mwaka baada ya mwaka, akatembea, akikiri, “Chochote kinyume na Hilo, hakikuwa—hakikuwa sahihi. La, bwana. Ilibidi iwe Hivyo. Mungu alisema hivyo.”

174 Nawazia baadhi ya adui zake wakikaribia, wakisema, “Baba wa mataifa, una watoto wangapi sasa?”

175 “Haileti tofauti yoyote jinsi nilivyo nao sasa. Mimi ni baba wa mataifa. Hivyo tu.”

“Unajuaje?”

176 “Mungu alisema hivyo. Hilo latosha. Hayo tu ndiyo yote kulihusu. Mungu alilisema, na hilo latosha.”

177 Kwa hiyo Ibrahimu akaendelea mbele. Ndipo hatimaye akafikia kwenye ile ninii halisi...halafu, mnaona, akiwa mwaminifu sana; mwaminifu zaidi, majaribu zaidi. Mnaona? Kwa hiyo akamrudisha moja kwa moja nyuma.

178 Sasa, kumbukeni. Wakati...Mungu amekuhesabu unastahili wakati ukiwa na jaribio. Sasa, msikose hili, kupata hili. Unapokuwa na jaribio ama kupimwa, inaonyesha neema ya Mungu imepata, umepata kibali kwa Mungu, naye Mungu anaamini ya kwamba utastahimili jaribio hilo.

Kumbuka, Yeye alifanya jambo lilo hilo kwa Ayubu.

179 Shetani alisema, “Loo, naam, nimemwona Ayubu kule chini.” Kasema, “Yeye si ninii...”

180 Mungu alisema, “Yeye ni mtumishi mkamilifu. Hakuna mwingine duniani kama yeye. Hakuna mtu kama Ayubu. Yeye ni mtu mkamilifu. Sasa, yeye, yeye ndiye ninii Yangu—yeye ni fahari na furaha Yangu.”

181 Shetani akasema, “Loo, hakika. Yeye hupata kila kitu aombacho.” Kasema, “Hebu nimpate mara moja.” Kisha akasema, “Mimi, nitamfanya akukufuru mbele za uso Wako.” Kasema, “Nitamfanya tu akukufuru.”

182 Mungu akasema, “Yuko mikononi mwako, bali kamwe usiuchukue uhai wake.” Mnaona? Mungu alikuwa na imani na Ayubu. Amina.

183 Wakati inapoonekana kana kwamba kila kitu kimeenda kombo, Mungu anakupa jaribu. Yeye ana imani nawe. Haimbidi kukubembeleza-bembeleza. Wewe si mmea kwenye kitalu, chotara. Wewe ni Mkristo halisi. Mungu anakupa jaribu, aone yale utakayofanya kulihusu. Amina. Si ajabu Petro alisema, “Majaribu haya yaliyo kama moto, mbona, yahesabu kuwa ni furaha. Ni—ni ya thamani kwako kuliko dhahabu.”

184 Na mara nyingi tunajizingira na kuvuma, “Loo, vema, laiti ningeninii tu...” Vema, hilo, vema, hicho ni kitu ulichopewa na Mungu, kushinda. Yeye—Yeye—Yeye anajua utashinda. Yeye, Yeye a—Yeye ameweka matumaini Yake juu yako.

¹⁸⁵ Naye alimwamini Ibrahimu... Ibrahimu alimwamini Mungu, hasa. Naye Mungu akasema, hapana shaka, alimwambia Shetani, "Ninaweza tu kukuthibitishia, yeye ananipenda." Kasema, "Mimi... Yeye anaamini ahadi hiyo, kwa sababu nilimwambia hilo." Kwa hiyo akampandisha mwanawe juu, juu ya mlima, akaifunga mikono yake nyuma yake, ile, ile siku Mungu aliyosema hivyo.

¹⁸⁶ Maskini Isaka akawa na shaka, mwajua. Akasema, Mwanzo 22, akasema—akasema, "Baba?"

Akasema, "Mimi hapa, mwanangu."

¹⁸⁷ Akasema, "Hizi hapa kuni, na haya hapa ma—ma—madhabahu, na kila kitu. Bali—bali—bali yupo wapi mwana-kondoo," unaona, "kwa ajili—kwa ajili—kwa ajili ya sadaka?" Akaanza kujisikia kidogo visivyo kawaida. "Haya—haya yote yanahusu nini? Sisi, tumeacha kitu fulani."

¹⁸⁸ Haileti tofauti yoyote yale unafikiri umeacha. Umeacha ushirika wa mengine yote. "Vema, huna budi kuwa na karamu zako za karata. Huna budi kufanya *hivi*. Inakubidi kunywa pombe kidogo. Nawe umeacha..." Hujaacha chochote. Endelea, litii Neno. Unaona? Hivyo tu, litii Neno tu. Hujasahau chochote. Litii tu Neno.

¹⁸⁹ Yeye akasema, "Mungu alisema, 'Mpandishe hapa juu,' naye ange—angeninii... Akapanda hapa juu ya mlima. Ninapaswa kufanya jambo fulani. Nitakapofika pale, nitalifanya."

¹⁹⁰ Kwa hiyo akapanda kule juu, na kuifunga mikono yake, kisha akamweka juu ya madhabahu, namna *hiyo*. Maskini Isaka hakunung'unika; mtiifu, mnaona, mfano wa Kristo. Ndipo alipotoa kisu kutoka kwenye ala yake, na kuvuta nywele zake nyuma kutoka usoni mwake, auchukue uhai wake, hiyo ilikuwa ndiyo siku ya Ibrahimu ya Ushindi; loo, jamani, wakati yeye, alipojaribiwa kufikia kwenye kiwango hicho, juu ya mwanawe wa pekee.

¹⁹¹ Sasa, kama wewe ni wa kiroho tu, peleka hilo kwenye jaribio, wakati Mungu alipomtoa aliye Wake Mwenyewe, unaona, siku ya Ushindi, yule aliyempenda. Mungu aliipenda sana jamii ya Adamu iliyoanguka! Tatalifikia hilo katika muda mfupi.

¹⁹² Angalia, siku ya Ushindi, siku ya Ushindi ya Ibrahimu ilikuwa kwenye Mlima Yire, ambako Mungu alimtolea sadaka badala ya mwanawe. Upendo, mnaona, upendo. Siku hiyo, Ibrahimu alimthibitishia Mungu, pasipo na kivuli cha tashwishi, uaminifu wake. Ibrahimu alithibitisha kwa Mungu, imani yake ndani Yake, kwa kuwa alisema, "Nilimpata mvulana huyu nilipokuwa na umri wa miaka mia moja, kwa kuamini ahadi. Na Yeye aliniambia nilikuwa baba wa mataifa. Kama akiniagiza kuutoa uhai wake, Mungu anaweza kumfufua kutoka kwa wafu." Whiu! Jamani, loo, jamani! Hilo linapaswa kumfanya Mpresbiteri apige makelele, sivyo? Mnaona? "Jinsi

ambavyo Yeye—Yeye—Yeye alivyonipa ahadi, na Yeye—Yeye—Yeye akanionyesha sasa thi—thibitisho la hili. Amina. Yeye, amenithibitishia hilo, ya kwamba Yeye hutimiza Neno Lake.”

¹⁹³ Vema, Yeye alitupata wapi? Nilitoka kwenye mchafuko wa jinsi gani? Wewe ulitoka kwa wa namna gani? Mawazo yetu yako wapi asubuhi ya leo? Ni kitu gani Yeye amethibitisha kuwa miongoni mwetu? Hakuna shaka kulihusu. Amina. Nayo si—siku yetu ya Ushindi ni ya hakika. Hatuna budi kuwa nayo. Mnaona? Yeye amelithibitisha.

¹⁹⁴ Ibrahimu anasema, “Yeye alinithibitishia. Nilikuwa sina mtoto. Nilikuwa—nilikuwa mzee. Nilikuwa tasa, na tumbo la uzazi la mke wangu lilikuwa limekufa. Nasi tulikuwa... Yeye alikuwa na sitini na mitano, nami nilikuwa na sabini na mitano, bali Mungu alisema, ‘Nitakupa mtoto kwake.’ Hilo lilitosha. Hayo yalikuwa ndiyo yote kwake.” Ibrahimu anasema, “Nililiamini.”

¹⁹⁵ Ndipo Mungu akamtupa kwenye miaka ishirini na mitano ya jaribio. Haikumaanisha kitu kwa Ibrahimu. Aliibuka mwenye nguvu zaidi kuliko alivyokuwa hapo mwanzoni, angali akimsifu Mungu. Hapana shaka, Mungu aliangalia chini na kusema, “Ni mtumishi wa jinsi gani!”

Kasema, Shetani alisema, “Loo, naam.”

Akasema, “Yeye...”

¹⁹⁶ “Lakini nita—nitathibitisha kwamba yeye ananipenda. Mpandishe kule juu, juu ya kilima, angamiza ushahidi wenyewe. Mpandishe kule juu.”

Naye Ibrahimu akapanda akalifanye. Hiyo ni kweli.

¹⁹⁷ Basi Ibrahimu, wakati alipoanza kuutoa uhai wa mtoto wake, Roho Mtakatifu akaunyakua mkono wake, kasema, “Ibrahimu, ondoa mkono wako. Ninajua unanipenda.” Amina.

¹⁹⁸ Huyu ndiye aina ya mtu ninayetaka niwe, kumpenda Mungu hata iweje. “Ondoa mkono wako.” Anakupa jaribu, ambapo hata ni kinyume na mawazo yako mwenyewe. Lakini, mradi tu Neno lilisema hivyo, lifanye, haidhuru. Mnaona?

¹⁹⁹ “Ondoa mkono wako. Ninajua ya kwamba unanipenda, maana hata hujanizuilia mwanao wa pekee.” Kasema, “Baraka, nitakubariki,” kasema, “uzao wake utasimama kwenye lango la adui, naye atashinda.” Loo, jamani! Alishinda, pia.

²⁰⁰ Baadaye kidogo, tutaupata huo “uzao wa Ibrahimu” pale. Vema. Ni nini...

²⁰¹ Mashaka yalikuwa yamemwondokea Ibrahimu. Wakati alipolisikia Neno halisi, mashaka yaliondoka. Wakati alipomwona Mungu akilithibitisha Neno, mashaka yaliondoka. Upendo ukachukua mahali pake. “Ninajua unanipenda, Ibrahimu. Hunitilii shaka hata kidogo. Haidhuru ilikulazimu

kungojea muda mrefu jinsi gani, ungali uliniamini. Nilikuagiza uangamize ushahidi wenyewe niliokuwa nimekupa. Nikupe ushahidi, kisha nikuagize uangamize. Nawe unanipenda vizuri sana, unalitii Neno Langu haijalishi ni nini.” Amina. Hiyo ilikuwa ni siku halisi ya Ushindi kwa Mungu. Mnaona?

²⁰² Yakobo alikuwa na siku ya Ushindi wakati mmoja. Aliogopa kurudi kwa ndugu yake, kwa sababu alikuwa ametenda uovu. Lakini, hata hivyo, Roho Mtakatifu akaanza kumwonya, moyoni mwake, “Rudi katika nchi ya uenyeji wako ulikotoka. Ulitoka katika nchi ya uenyeji. Ulifanya uovu huko, sasa ninakurudisha.” Ndipo alipokaribia, alipata... Hakika, bila shaka.

²⁰³ Hilo ndilo ibilisi analotufuatia sana. Mnaona? Hilo ndilo ibilisi analomfuatia sana Bibi-arusi, Kanisa, kwa hiyo, kwa sasa, siku ya Ushindi inakaribia. Hiyo ni kweli. Inakaribia sana. Hapo ndipo adui anapofanya mabaya awezayo, kupanga askari wake tena. Biblia ilisema, “Ole kwa dunia, kwa maana ibilisi ni kama simba angurumaye, katika siku za mwisho, akizungukazunguka, akimeza atakacho,” mnaona. “Ole wao”; mateso na kadhalika yatatokea. Shikilia moja kwa moja Kwake. Kamwe usisogee, kulia wala kushoto. Dumu moja kwa moja na hilo Neno. Mungu alisema hivyo. Hilo latosha.

²⁰⁴ Yakobo, akitamani moyoni mwake, kila kitu kilionekana ni kibaya. Alitaka kurudi nyumbani. Roho Mtakatifu alikuwa akimwongoza. Alikuwa amefanya ahadi kwa Mungu. Ilimbidi kwenda Betheli, kutoa hizi zaka na kadhalika. Basi hapa, akiwa njiani akirudi, anakuta kwamba Esau, ndugu yake adui, alikuwa—alikuwa tu ng’ambo ya pili ya mto, akimngojea, pamoja na jeshi. Kwa hiyo, Yakobo alikuwa ni mwoga, hata hivyo alikuwa na baraka za Mungu. Mungu alikuwa ameahidi kumbariki. Alikuwa na haki ya mzaliwa wa kwanza. Amina.

²⁰⁵ Ni mfano jinsi gani wa kanisa leo hii, pamoja na ubatizo wa Roho Mtakatifu, pamoja na ahadi ya Neno la Mungu kulithibitisha, kwa sababu wewe unafanyika sehemu ya Neno hilo, ile haki ya mzaliwa wa kwanza.

²⁰⁶ Naye Yakobo alikuwa na haki ya mzaliwa wa kwanza. Amina. Alikuwa... Ndugu yake hakuijali. Naye alikuwa na haki ya mzaliwa wa kwanza, kwa sababu ndugu yake alimwuzia kwa supu ya dengi.

Vivyo hivyo ulimwengu wa kanisa leo hii umeuza haki yao ya mzaliwa wa kwanza.

²⁰⁷ Basi Mungu ashukuriwe, tunayo. Naam. Tunayo. Tunajali nini kuhusu umoja wa makanisa, na Shirikisho la Mataifa, na mambo haya mengine yote, mradi tu una haki ya mzaliwa wa kwanza?

²⁰⁸ Kile kanisa linachohitaji kufanya, ni kufanya kama Yakobo, kuomba mpaka upate siku ya Ushindi. Na, kweli,

Yakobo alikuwa na karamu ya kupiga mwereka. Alipigana mwereka usiku kucha, na Bwana, bali akasema, “Sitakuacha tu uondoke mpaka nitakapopata ushindi huu.” Ndipo basi karibu mapambazuko, asubuhi moja, akapata siku ya Ushindi. Hakutembea vile vile, tena. Lakini, upande *huu*, yeye alikuwa tu ni mfuasi wa kanisa mwoga, mkubwa mno, mwenye nguvu. Lakini, ng’ambo ya pili, alikuwa maskini kuhani, ama mtawala, hasa, anayechechemaa; maskini mtawala anayechechemaa, mwenye ujasiri wa kutosha kupigana na jeshi zima.

Esau akasema, “Nitakuandalia jeshi.”

Akasema, “Sina haja nayo.” Alikuwa amepata siku ya Ushindi.

²⁰⁹ Hatuhitaji madhehebu yao. Hatuhitaji vitu vyao—vyao vya ulimwengu huu. Hatuhitaji ninii zao...kuhitaji kupatana katika mambo ya ulimwengu huu. Tumekuwa na siku ya Ushindi. Tulipiga mwereka siku moja, ama usiku mmoja.

²¹⁰ Loo, jinsi ninavyokumbuka ule mwereka, wakati—wakati iliponibidi kufa kwa nafsi yangu. Lakini palitokea siku ya Ushindi, wakati nilipopata ushindi, ndipo Neno la Mungu likawa ni kweli. Kanisa la Kibaptisti, kwangu mimi, halikuwa zaidi ya dhehebu lolote lingine. Hiyo ni kweli. Nilikuwa na siku ya Ushindi. Neno la Mungu ni kweli.

Dk. Davis alisema, “Mbona, utakuwa mtakatifu anayejibingirisha.”

Nikasema, “Mtakatifu anayejibingirisha, ama si mtakatifu anayejibingirisha!”

²¹¹ Juu, huko chini kwenye Kinu cha Green, nilikaa usiku kucha katika maombi, mpaka Malaika huyo akaingia pale asubuhi hiyo, ile Nuru. Kasema...Nini? Nilikuwa nikijaribu kuondosha kitu kile hasa ambacho Mungu alinipa kupiga vita nacho, yale maono, wakati walipokuwa wakiniambia yalikuwa ni ya ibilisi. Ndipo Yeye akaja, akiniambia, akirejea kwenye Maandiko, “Hivi hawakusema jambo lile lile kuhusu Mwana wa Mungu, na kadhalika?” Nilikuwa na siku ya Ushindi. Hamna mengine ya hayo kwangu mimi. Nikaingia hudumani, na kuzunguka na kuzunguka ulimwengu. Siku ya Ushindi!

²¹² Mnaona, Yakobo alikuwa na hii siku ya Ushindi. Alipiga mwereka, usiku kucha. Lakini wakati siku ilipoanza kupambazuka, ilikuwa ni siku ya Ushindi kwake.

²¹³ Ushindi huu wote mkuu na kadhalika! Tukianza kuzungumzia mambo haya, hamna mahali pa kusimamia, siyoy? Ushindi huu wote mkuu ulikuwa ni sawa. Tunauthamini kila mmoja. Wote ulikuwa ni ushindi mkuu. Ule ushindi mkuu wa vita, na ushindi mkuu wa vita vya kiroho, na kadhalika, ulikuwa ni mkuu. Lakini, mnaona, hakuna mmoja wao uliokuwa

ni wa kudumu. Mnaona? Tunao ushindi mkuu, usiodumu. Sasa, tuninii tu. . .

²¹⁴ Tulipata huku nje, sio muda mrefu uliopita, tulipoenda vitani na Japani. Mbona, mimi—mimi. . .nyumbani mwetu, kulikuwako na kifaa kidogo. Mtu fulani alikuwa ametupa kidogo, loo, kipambo, mwajua, kidogo kama mwanasesere. Nacho kilikuwa kimeandikwa, “Kimetengenezewa Japani.” Jamaa huyo akakitupa chini na kukivunja. Mnaona? Nawe ungesema, “Kimetengenezewa Japani,” wangekitupa nje. Ama, wanaenda katika maduka ya bei rahisi, kundi la kina Riki, mwajua. Sio kwamba. . . Watu wahalifu huenda mle, duka la bei rahisi, kujifanya tu werevu, mnaona, wanaingia na kuchukua vitu kutoka Japani. Walitaka kuonyesha uaminifu wao kwa taifa fulani.

²¹⁵ Vipi kuhusu Mungu? Wanacheka usoni Mwake. Mnaona? Kama ilikuwa ni rahisi sana kwao kuingia mbio kwenye duka la bei rahisi na kuangusha makaunta, na vitu kama hivyo, kwa kuwa walikuwa na wanasesere wadogo na vipambo, na kadhalika, hivyo vilivyotengenezwa kutoka. . . vilivyotengenezewa Japani, kwa sababu walikuwa katika vita nao; vipi kuhusu kuvuta sigara, na kunywa pombe, kudanganya, kuiba, na mambo kama hayo, mnaona, kwa jeshi halisi la Mungu? Mnaona? Wanataka kuwa waaminifu. Vipi kuhusu sisi kuwa waaminifu? Kama walipelekwa gerezeni kwa kufanya hivyo, ilileta tofauti gani? Wanataka kuwa waaminifu kwa taifa, kwa bendera. Ila Mkristo anaogopa, wakati mwingine, ku sema waziwazi. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu tunahitaji siku nyingi zaidi za Ushindi, wakati unapoweza kuifanya nafsi yako ishindwe. Unaona? Acha Mungu akushinde kwa nguvu Zake za upendo.

²¹⁶ Ushindi huu wote mkuu ulikuwa ni ushindi usiodumu. Hata, kwa Musa, Israeli ilirudi moja kwa moja katika utumwa tena. Sikuzote, kuingia na kutoka, kuingia na kutoka, tunawaona. Mashujaa wengi wangali waliendelea kupiga vita, na kufa. Wangali wanafanya hivyo katika vita, katika fokasi ya kawaida ya darubini. Wanafanya hivyo katika kiroho. Mashujaa hupigana na kufa. Jinsi ambavyo tungeshuka chini. Nina mlolongo mzima wao ulioandikwa hapa, kama vile Danieli, na wale wana wa Kiebrania, na hao washindi wakuu huko nyuma waliopata ushindi.

²¹⁷ Lakini wao kila mara. . . hatimaye kikaja kitu kilichoitwa mauti, kikawachukua, mnaona, haidhuru. Wakaendelea moja kwa moja, mnaona, wangali wakipiga vita, wakifa; wakipiga vita, wakifa; wakipata ushindi, wakifa; wakipata ushindi, wakifa.

²¹⁸ Lakini, mnaona, hata hivyo, mwanadamu hakuumbwa apate kufa. Mwanadamu aliumbwa apate kuishi. Na haidhuru ni

mafanikio mangapi aliyopata, bado alikufa, haidhuru. Basi walipoenda kaburini, walimzika, na hilo likalimaliza. Walitia alama kaburi lake kwa jiwe la kaburi huko nje, na, ama, kaburi lake, na huo—huo ulikuwa ndio mwisho wake. Mauti yalimmeza. Yule Musa mashuhuri, Yoshua mashuhuri, manabii mashuhuri wa Biblia, karibu wote, ila yapata wawili ama watatu, tunajua mahali makaburi yao yalipo, ambapo liliyatia alama. Mauti yaliwameza na kuwapeleka moja kwa moja. Mnaona?

219 Lakini siku moja, vilitokea vita, hapo Shujaa Mkuu wa Vita akashuka akaja, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Basi kulikuwako na Pasaka. Hiyo ilikuwa ndiyo siku ya Ushindi halisi, baada ya Yesu kupiga vita na kushinda. Alipiga vita dhidi ya kila adui aliyekuwako wa kupigana naye.

220 Jambo la kwanza, wakati alipozaliwa, Alizaliwa na jina chafu, kwanza, miongoni mwa watu, kama Mwana haramu. Alipiga vita Mwenyewe moja kwa moja kupitia hilo. “Mariamu, kumpata mtoto huyu kwa Yusufu, pasipo kufanya ndoa.” Alikuwa miongoni mwa watoto wadogo, akiwa na jina. Lakini, moyoni Mwake, Yeye alijua alikuwa ni Mwana wa Mungu. Mnaona? Alipiga vita kupitia hilo.

221 Alifika kwenye siku ambapo angefanya maamuzi Yake ya yale aliyotaka kufanya, akiisha kumpokea Roho Mtakatifu.

222 Aliifikia siku ambapo Shetani alimpeleka juu ya mlima, naye akamwonyesha falme zote za dunia, na kusema, “Nitakufanya mfalme sasa. Unasema Wewe ni Mwana wa Mungu, na unazo nguvu. Nitakupa mtawala juu ya mataifa yote,” kile tu mpinga Kristo anachojaribu kuwa siku hizi. Lakini kulikuwako na siku ya Ushindi. Alipiga vita moja kwa moja kupitia hilo. Kasema, “Ikiwa Wewe ni Mwana wa Mungu...”

223 Ukaja wakati ambapo alipewa changamoto kwenye Neno. “Ikiwa Wewe ni Mwana wa Mungu, yaamuru mawe haya yafanyike mkate.” Mnaona? “Na Wewe una njaa, sasa yale.” Mnaona? “Ikiwa Wewe ni Mwana wa Mungu, unaweza kufanya hivyo.” Angeweza kufanya. Hiyo ni kweli. Lakini ilibidi kuwe na siku ya Ushindi. Alipata ushindi juu ya jaribu hilo. Mnaona? Alishinda ninii. . .

224 Kasema, “Sasa Wewe unaweza kuwa Mtu mashuhuri. Unaweza kujionyesha Mwenyewe, kile ulicho Wewe.” Akamchukua, kinara, hekalu, kasema, “Jitupe chini. Nitakunukulia Maandiko, Imeandikwa, ‘Atakuagizia Malaika, usije ukajikwaa mguu Wako katika jiwe wakati wowote, nao watakuchukua.’” Angalieni huyo mwanatheolojia Shetani alivyo. Mnaona?

225 “Rudi nyuma Yangu, Shetani,” likaja Neno. Ilikuwa ni siku ya Ushindi. Yeye alikuja kwenye kila siku ya Ushindi.

²²⁶ Akaenda mbele za—za mama ya mke wa Petro amelala pale, anaugua homa. Homa ilikuwa ikiushambulia mwili wake. Walihitaji huduma. Anaenda pale na kuugusa mkono wake. Maradhi yasingeweza kuhimili Uwepo Wake. Hakika yasingeweza.

²²⁷ Kisha akaja mahali ambapo kulikuwako na mauti katika—katika familia moja. Akaja mahali ambapo mtu jina lake Lazaro, rafiki Yake, alikuwa amekufa na akazikwa, naye amelala kaburini, huku ananuka, yapata siku ya nne. Mwili huingia uharibifu katika siku tatu, mnaona, saa sabini na mbili, uharibifu. Ndipo pakafikia mahali ambapo uzima na mauti yalikabiliana. Huyu hapa, Uzima; pana mauti, yaliyomchukua rafiki yake; katika shindalo la kuamua. Akaenda kaburini, akayavuta maskini mabega hayo nyuma, kasema, “Lazaro, njoo huku.” Loo, jamani! Hilo Neno likatolewa. Lilikuwa ni Neno la Mungu. Uzima ukajirudia wenyewe tena. Mwathiriwa akarudi, kutoka ng’ambo ya ng’ambo, mahali fulani, akawa hai tena. Hakika. Alipata ushindi. Hiyo ni kweli.

²²⁸ Maradhi, majaribu, kila kitu kingaliweza kuwa, Yeye alipiga vita kupitia kila kimoja. Siku ya Ushindi! Kweli kabisa.

²²⁹ Ndipo ukafika wakati ambapo ulimwengu mzima ulikuwa umekaa kwenye vivuli, maeneo ya vivuli vya mauti; kila mtu, kila mwanadamu, kila nabii, kila mtu mashuhuri, mashujaa hawa wote mashuhuri aliokuwa amewatuma. Wote walilala huko nyuma. Kulikuwako na Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Yusufu, hao wote wamelala kaburini huko nyuma, wakiamini; hamna ushahidi zaidi ila tu, “Neno la Mungu lilisema hivyo. Mungu alisema hivyo.”

²³⁰ Mtazameni Ayubu wakati alipokuwa akipiga vita kwa nguvu sana. Mke wake, hata mke wake, mwenziwe, alisema, “Hata pumzi yake imekuwa ni ngeni kwangu,” kadhalika. Alikuwa. . .

²³¹ Ni wakati wa jinsi gani mtu huyo aliokuwa nao, hayo majaribu! Na hata kwa Belzari na hao wengine wote, walisema, hata na Elihu, walijaribu kumshtaki, na mambo kama hayo. Lakini yeye alijua alidumu pamoja na Neno.

²³² Ndipo mke wake akaja na kusema, “Ayubu, unaonekana mwenye taabu.” Kasema, “Kwa nini usimkufuru tu Mungu ukafe kifo?”

²³³ Akasema, “Unazungumza kama mwanamke mpumbavu.” Aha! Loo, jamani! Ni shujaa jinsi gani!

Hata Yesu alirejea kwake, “Hamjasikia habari ya subira yake Ayubu?”

²³⁴ Ayubu aliaga dunia angali vitani. Ibrahimu aliaga dunia angali vitani. Naam, bwana. Isaka aliaga dunia akiwa vitani. Yusufu aliaga dunia akiwa vitani.

235 Yusufu alisema, “Msinizike hapa chini, hata hivyo. Nizikeni hapa juu, mnaona, nizikeni hapa juu pamoja na baba zangu. Nizikeni jinsi walivyozikwa, Neno, uwanda waliozikiwa, mahali walipozikwa.”

236 Hilo ni jambo lile lile ndani yangu. Hiyo ndiyo sababu ninataka kuzikwa katika Jina la Yesu. “Kwa kuwa wale walio katika Kristo Mungu atawaleta pamoja Naye,” mnaona.

237 Kwa hiyo basi tunaona, kuendelea na kuendelea na kuendelea, wakaondoka hao mashujaa, mashujaa, mashujaa. Ndipo hapa ukaja wakati ambapo Jemadari Mkuu, aliyekuwa amewatuma . . . Nao walikuwa wameanguka kwenye uwanja wa vita, washindi wakuu. Wakafikia kwenye siku zao za Ushindi, nao wakapata ushindi dhidi ya adui. Hata walininii . . .

238 Yoshua, pamoja na . . . alikuwa na . . . akitaka muda, alilisimamisha jua kwa neno lake mwenyewe, wala halikuwaka. Nalo jua halikutua kwa saa ishirini na nne. Biblia ilisema, “Hapakuwapo na mtu, hapo kabla ama baadaye, aliyepata kuliamuru jua kusimama kimya, ambapo Mungu aliisikia sauti ya mwanadamu.”

239 Kwa nini? Mnaona, alimshinda adui kabisa. Mnaona? Walikuwa ninii tu, walikuwa wamefurushwa kabisa, kila mahali. Ilimbidi kuwawinda na kuwaua. Hayo ndiyo yote yaliyokuwako kulihusu, kwa sababu hilo lilikuwa ndilo agizo lake. Naye alijua, kama ingewahi kufika majira ya usiku, wangepata wakati wa kuhamasisha tena na kukusanyika pamoja, naye angewapoteza watu wengi zaidi. Kwa hiyo akasema, “Ninahitaji muda. Ninahitaji mwangaza. Jua, simama kimya.” Amina. Ee Mungu. Mungu alisikia neno la mwanadamu na kulisimamisha jua. Lilikaa mahali pake pale pale kwa muda wa saa ishirini na nne, mpaka akapiga vita, akamtoa kila mmoja wa adui na kuwaangamiza. Wasingeweza . . . Hakuwapa nafasi ya kujihamasisha tena. Aliendelea kusonga mbele.

240 Na, hata hivyo, Yoshua aliuweka uhai wake chini, amelala katika mavumbi ya nchi.

241 Lakini wakati huyu Mtawala mkuu alipokuja, Kristo, Yule ambaye Danieli aliona . . .

242 Yule shujaa mkuu wa vita, Danieli, katikati ya shida zote na vitu kama hivyo, na ninii kuu . . . Ambapo, kama tungalikuwa na wakati, tungemrejea. Hata hivyo, yeye alilala kwenye mavumbi ya nchi. Akasema, “Utastarehe katika awamu yako siku hiyo, lakini, Danieli, utasimama tena.”

243 Sasa, ahadi ambayo alikuwa amepewa, kwa mashujaa hawa wote, mpaka, hatimaye, wakati ukaja, na ile saa muhimu, kwamba haina budi kulipwa. Yesu alikuwa amekuwa duniani. Alikuwa ameshinda kila maradhi. Alishinda kila kitu. Sasa hana budi kulishinda kaburi.

244 Alikuwa ameshinda mauti. Mauti yasingeweza kukaa Mbele Zake. Yeye kamwe hata hakuhubiri mazishi. La, bwana. Yule mjane wa Naini alitoka pamoja na mwanawe, namna hiyo. Yeye akalisimamisha, akamfufua. Loo, jamani! Naam, bwana. Yeye alithibitisha ya kwamba alikuwa na nguvu juu ya mauti.

245 Sasa kuna adui wengine wawili: hao ni kaburi huko nje, na kuzimu; jehanamu, kaburi. Kwa hiyo katika siku hiyo wakati Yeye alipokufa akawa mfu sana hata jua likaacha kuangaza, na dunia—dunia ilikuwa na mavundevunde kwa wasiwasi, mawe yakapopotoka vilimani, na vitu kama hivyo, Yeye akafa. Akashuka chini kuzimuni. Akayashinda mauti. Akashinda kuzimu. Kwenye asubuhi ya Pasaka Yeye akashinda kaburi. Amina.

246 Nena kuhusu siku ya Ushindi mkamilifu? Siku ya Ushindi halisi: Akawatoa nje. Na si hilo tu, bali, hapo alipotoka kaburini, aliwaleta wafungwa waliokuwamo humo. Biblia ilisema, “Aliwateka mateka.” Akatoka kaburini, akileta pamoja na Yeye, mashujaa hao wote huko ng’ambo. Hivi hamjui huo ulikuwa ni wakati mkuu huko juu siku hiyo, wakati wao—wakati walipoingia kwenye Ufalme huo, jamani, wakaingia katika Ufalme wa Mungu, akawaleta mateka watakatifu kutoka mle! Yeye alikuwa ni ushindi mkamilifu, ushindi mkamilifu. Aliwaleta mashujaa wote waliokufa. Aliwatoa Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Ayubu, na hao wengine wote, akawaleta kutoka kaburini pamoja Naye.

247 Akawateka. Mnaona, Yeye alikuja duniani, akateka mauti. Aliteka kuzimu. Akateka kaburi. Aliteka kila kitu. Na sasa anafufuka, amina, pamoja na watakatifu Wake pamoja Naye.

248 “Sasa alipaa Juu na kuwapa wanadamu vipawa.” Ilikuwa ni nini? Panga, akaweka panga mkononi mwao, Neno, mnaona, wapate kushinda. Loo, jamani! Aliwapa panga, (ya nini?) Neno, kushinda nini? Maradhi, dhambi, ushirikina, uovu, kuleta kila kiumbe kilicho hai kinachotaka kuishi, kumleta kila mmoja wao apate kutambua, ya kwamba, “Kwa kuwa Mimi ni hai, ninyi mu hai pia.”

249 Tuna vita vya imani. Na tupige vita ninii vizuri. . . Kumalizia ushindi wetu, kwa kuwa ushindi wetu mkamilifu ni hakika. Ni hakika. Hauna budi kuwa. Tuna malimbuko yake. Tunao ushahidi wake moyoni mwetu sasa, kwa sababu tayari tumeweka vita vyetu vya kwanza nyuma yetu. Tumeweza kushinda, kupitia Imani ya Yesu Kristo. Tulikuwa na siku ya Ushindi.

250 Ninakumbuka huko chini, kwamba yapata saa nne usiku mmoja, ama wakati nilipokuwa huko chini kwenye maskini gereji ile ya kale, nikiomba, “Mungu, niue ama uniokoe.” Nilienda makanisani. Walinitaka nipande juu na kupeana mikono na mhubiri.

Nikasema, “Ninataka kitu fulani zaidi ya hicho.” Unaona?

²⁵¹ Ndipo katika gereji hiyo usiku huo, wakati niliposema, “Mungu, siwezi kuendelea mbele zaidi. Ni—nitakufa.” Ndipo nilipokuwa huko katika maskini jengo hilo la kale, lililolowa maji, na magoti yangu. . . Nilikuwa nimepiga magoti juu ya gunia chakavu la nyasi, huku nimeinua mikono yangu juu, nikisema, “Mungu, sijui namna ya kuzungumza, Bwana.” Nilitaka kumwandikia barua, kumwomba anisamehe. Sikujua jinsi ya kuomba. “Ninataka nisamehewe.”

²⁵² Niliahidi hilo wakati nilipokuwa nikifa kitandani. Na Yeye akanijalia. . . Wakati daktari alikuwa amenikatia tamaa, moyo wangu ulikuwa ukidunda tu mara kumi na saba kwa dakika. Nanyi mnajua jinsi huko kulivyokuwa polepole. Akasema, “Yeye yuafa,” nami nikasikia hilo. Akamwambia baba yangu, kisha akafunga pazia kunizunguka. Na hapo katika chumba hicho, saa hiyo, niliziona hizo J kubwa zikija kila mahali; pazia hilo lilikuwa limenizunguka, namna *hiyo*. Nikamsikia nesi huyo akilia, akisema, “Yeye si kitu ila mtoto mdogo,” mnaona, “naye huyu hapa akiondoka.” Nusukaputi ya uti wa mgongo ilikuwa imevuja na kuingia moyoni mwangu. Mnaona? Ulikuwa ukipiga tu mara kumi na saba kwa dakika.

²⁵³ Nilipofika nyumbani, ilinibidi kuthibitisha ya kwamba, ya kwamba ni—nilimpenda Mungu. Ndipo ni—nikapiga magoti pale sakafuni. Nikasema, “Si—sijui jinsi ya kuomba.” Kisha ni—nikauma ukucha wa dole gumba langu. Nikawaza, “Labda. . . nimeona picha. Nitakunja mikono yangu namna *hii*, niweke vidole vyangu pamoja.” Nikasema, “Mpendwa Bwana, ningetaka kuzungumza na Wewe.” Ningesikiliza. Nikasema, “Sikusikii.” Nikasema, “Nilikunja mikono yangu vibaya. Labda ninapaswa kuifanya *hivi*.” Nikaweka ninii yangu. . . Nikasema, “Mpendwa Bwana, mimi. . . Yesu Kristo, ningetaka kuzungumza na Wewe.” Nikasema, “Bwana, sikusikii. Nijibu. Nimewasikia watu wengine wakisema, ‘Mungu alizungumza nami.’ Sasa ninataka kulizungumzia hili pamoja na Wewe. Nilikuahidi ningefanya hivyo. Ninataka kulizungumzia. Hivi utakuja na kuzungumza nami, Bwana?” Nikawaza, “La, siiweki mikono yangu vizuri, la sivyo Yeye angesema kitu.” Sikujua jinsi ya kulifanya. Sijawahi kuomba maishani mwangu. Sikujua la kufanya; maskini kibanda hiki cha kale.

²⁵⁴ Siku moja, basi, nikawazia jambo hili. Nikawaza, “Kulingana na Maandiko, kama vile nimeyasikia yakisomwa, Yeye alikuwa ni Mtu. Na kama alikuwa ni Mtu, Yeye anafahamu kama Mtu.” Hiyo ni kweli. “Na sasa, sijui kama Wewe unanisikia.”

²⁵⁵ Ibilisi akasema, “Mbona, wewe tayari umetenda dhambi ukaimaliza siku yako ya neema. Haipo tena. Unaona, umekuwa katili sana, hata Yeye hatakusamehe.”

256 Nikasema, “Siamini hilo. Kamwe siwezi kuliadini. Ninaadini Yeye angezungumza nami.”

257 Nikasema, “Bwana, sijui kama ninafanya kosa, kama sajaikunja mikono yangu vizuri, ama chochote kile, Wewe—Wewe nisamehe hayo. Lakini ninataka kuzungumza na Wewe.” Nikasema, “Mimi ndimi mhuni duni kuliko wote ulimwenguni.” Nikasema, “Mimi, mimi nimefanya mambo haya yote, na—na nikakukimbia Wewe, na yote,” nikaendelea kuzungumza namna hiyo.

258 Basi jambo la kwanza mwajua, nilipokuwa nikizungumza, Nuru ndogo ikapitia chumbani, ikaenda juu kando ya ukuta, na kufanya msalaba wa Nuru, ile Nuru, kisha ikaanza kuzungumza kwa lugha fulani. Kamwe, kamwe sikuwa nimesikia kitu kama kunena kwa lugha; hata sikuwa nimewahi kuisoma Biblia; Nilikuwa nikitafuta Yakobo 5:14 katika Mwanzo. Nilikuwa nikiangalia pale juu, ndipo nikaiona hiyo Nuru, Nayo ilikuwa ikizungumza namna fulani ya lugha. Kisha ikaondoka.

259 Nami nikasema, “Bwana,” nikasema, “Si—si—sijui chochote kuhusu maisha haya ya Kikristo.” Nikasema, “Kama—kama huyo alikuwa ni Wewe ukizungumza nami, siwezi kuelewa lugha Yako, Bwana. Lakini kama utazungumza... Na ikiwa huwezi kuzungumza lugha yangu, unaona, na mimi—mimi sielewi Yako, ila naomba tuelewane jinsi hii: iwapo utarudi tu pale tena, hiyo itakuwa ni ishara kati yangu na Wewe, ya kwamba utanisamehe.”

260 Hiyo hapo tena. Loo, ati mwanena kuhusu siku ya Ushindi? Nilikuwa na moja, naam, siku ya Ushindi halisi. Ilikuwa ndiyo Hiyo hapo tena, ikizungumza vile vile. Ndipo nikawa na siku ya Ushindi. Loo, jamani!

261 Na tangu wakati huo, wakati alipoliweka Neno mkononi mwangu, nimepiga vita kushinda tuzo, kuabiri katika bahari zilizojaa damu.

262 Sote tumepata ushindi. Tumepiga vita kupitia kwenye ushindi mwingi. Nao ushindi mkuu unakuja hivi karibuni tu, moja kwa moja kwenye kona. Siku yetu ya Ushindi mkamilifu itakuwa hivi karibuni, wakati Mwana wa Mungu atakapozipasua anga, na kutoa sauti kuu kwa Sauti ya Malaika Mkuu, na Yeye atakuja tena. Ndipo makaburi yatafunguka, na wafu watatoka nje.

263 Nafikiri ninyi hucheza kanda zangu hapa chini, juu ya lile ono ambalo ndiyo kwanza niwe nalo, ama kuhamishwa, chochote kilichokuwa, chumbani; na nikaenda kule juu na kuwaona watu hao, jinsi tu ninavyowaona ninyi, Biblia hii ikiwa wazi hapa mbele yangu. Naye Mungu anajua hilo ni kweli. Mnaona? Huko walikuwa ni vijana, kama tu na, kama...

264 Nyote mmekuwa mikutanoni, nanyi mnatambua, maono hayo. Mmepata kuona moja likishindwa? La, bwana. Hivi

majuzi tu Yeye alinituma hapa nje kwa moja, akaniambia kile kilichotukia. Ninyi nyote, nyinyi nyote, mnajua kulihusu. Nikaenda moja kwa moja. Lilikuwa papo hapo, kabisa. Halishindwi kamwe.

²⁶⁵ Nami ninawaambia, kama kundi dogo la Kikristo linaloketi hapa asubuhi ya leo, ushikilieni mkono wa Mungu usiobadilika. Mmekuwa na ushindi usiodumu. Lakini inakuja siku halisi ya Ushindi, kamilifu, wakati Yesu atakapokuja.

²⁶⁶ “Ndipo parapanda italia; waliokufa katika Kristo watafufuka.” Basi ikiwa huna tumaini hilo ndani yako, usiache siku hii ipite pasipo kulipata.

²⁶⁷ Nilisikia kitu fulani kidogo, muda mfupi uliopita, ningetaka kurudia. Kilitoka, naamini, ilikuwa ni Billy Sunday aliyetoa tamshi hilo. Kulikuwako na mvulana aliyekuwa amefanya uhalifu. Sijui kama mmewahi kuisikia, ama la. Alikuwa amefanya uhalifu. Wakamtupa gerezani, naye alikuwa anaenda ku... Alikuwa ndani. Na kwa hiyo alifanyiwa kesi. Basi—basi hakimu akasema... .

²⁶⁸ Ndipo baraza la wazee wa mahakama likaja na kusema, “Tunampata mvulana huyu na hatia ya uhalifu huo. Nasi,” baraza la wazee wa mahakama likasema, “tunaomba uhai wake.”

²⁶⁹ Ndipo hakimu akasema, “Na—nakuhukumu kufa, kuning’inizwa kwa kamba, mpaka uhai wako wa kibinadamu umeondoka. Basi Mungu na airehemu nafsi yako.”

²⁷⁰ Basi mvulana huyo akapelekwa gerezani, akawekwa kwenye jela la ndani, kwamba ingembidi kukaa huko mpaka wakati wa kufa kwake.

²⁷¹ Ndipo marafiki wakamjia hakimu, na kusema, “Hakimu, tulichangia kukuchagua hapa mjini. Tafadhali, tafadhali, usiache jamaa huyo mdogo afe namna hiyo.”

²⁷² Ndio kwanza nitoke Texas, kwa nyingine, jambo kama hilo. Kijana mwanamume na kijana mwanamke, naye Mungu akayaokoa maisha yao. Walikuwa wafe, yapata siku tatu ama nne baadaye. Nadhani nyote mliliona hilo gazeti, mlikuwa pamoja nami huko, kwamba waliyaokoa maisha yao.

²⁷³ Kwa hiyo wakasihi, na kusihi, na kusihi, hao watu, kwamba asifanye hivyo. Kwa hiyo baada ya kitambo kidogo, kwa gavana wa jimbo... .

²⁷⁴ Mama, nje ya mlango, siku moja, alianguka chini mlangoni, namna *hiyo*, na kulia apate kuingia.

²⁷⁵ Ndipo hatimaye mtu huyo akaingia, kasema, “Mama ya yule mvulana, gavana, yu—yuko nje pale. Anataka kukuona.”

Ndipo gavana akasema, “Mlete ndani.”

²⁷⁶ Basi mwanamke huyo, katika unyenyekevu, alitambaa kwa mikono yake na miguu, mpaka kwa gavana, akavishika viatu vyake, na kusema, “Bwana, huyo ni mtoto wangu. Usimwue. Usimwue. Ndiye wa pekee tu niliye naye. Usimwue.” Kasema, “Hakumaanisha kufanya hivyo. Mpe tu kifungo cha maisha gerezani. Bali usiyachukue maisha yake, gavana.”

Gavana akasema, “Vema, nitaenda huko chini nikamwone.”

Kasema, “Vema.”

²⁷⁷ Kwa hiyo gavana akashuka kwenye seli alimokuwa, nao wakaingia. Mvulana huyo alitaka kuwa na kiburi. Kasema, “Kuna mtu amekuja kukuona.”

²⁷⁸ Ndipo gavana akaingia, kasema, “Kijana, ningetaka kuzungumza na wewe.” Akashikwa na kiburi kabisa, akaketi tu chini, amefunga mdomo, asingesema chochote. Akasema, “Kijana, ninataka uzungumze na mimi. Nataka kuzungumza na wewe.” Naye mvulana huyo akafanya kana kwamba hata hakumsikia. Naye akasema, “Kijana, ninaweza kukusaidia kama utaniruhusu.”

²⁷⁹ Kasema, “Toka hapa. Sitaki kusikia lolote unalotaka kusema.”

Akasema, “Vema, mwanangu . . .”

²⁸⁰ Akasema, “Nyamaza. Hivi huoni kwamba nina fadhaa? Sitaki kusikia neno moja utakalosema.”

Akasema, “Vema, nilikuja . . .”

Akasema, “Toka kwenye seli hii.”

Kwa hiyo akatoka. Wakafunga milango.

²⁸¹ Kwa hiyo aliporudi, yule jamaa, po—polisi kwenye ulinzi, mlangoni, kasema, “Wewe ndiye mtu mpumbavu kuliko wote.”

Akasema, “Huyo mwendawazimu alikuwa ni nani, hata hivyo?”

Akasema, “Huyo alikuwa ni gavana wa jimbo.”

²⁸² Kasema, “La, sio gavana. Mtu pekee anayeweza kunisamehe, nami nimemfukuza kutoka seli yangu. Mtu pekee anayeweza kutia sahihi msamaha wangu, nami nimemfukuza kutoka kwenye seli.”

Wakati gavana akitoka nje, alisema, “Alifanya chaguo lake.”

²⁸³ Kwa hiyo, jambo la mwisho mvulana huyo alilosema, wakati walipomvisha ile hijabu nyeusi juu ya uso wake, ili kumnyonga, walipoivuta kamba wakaikaza, wakaweka hijabu juu yake, alisema, “Wazieni jambo hilo. Gavana alisimama katika seli yangu na angenisamehe kama sikumfukuza.”

²⁸⁴ Tunajuaje, asubuhi ya leo, ya kwamba Gavana hasimami karibu na seli yetu asubuhi ya leo? Usimfukuze, ikiwa kamwe hujawahi kupokea msamaha kutoka Kwake. Sio tu Gavana,

bali Mfalme, Yule pekee Ambaye anaweza kukusamehe, huenda amesimama karibu na seli hiyo ndogo ambamo umekuwa ukiishi kwa muda mrefu. Kwa nini usimruhusu tu aingie, ikiwa huja—hujafanya hivyo, kama hujajitolea kikamilifu Kwake?

²⁸⁵ Siku moja, utakuta kwamba njia hii ndogo nyenyekevu, ambayo huenda ukawazia ni lundo tu la upumbavu, kundi la watu ambao hawajui wanalozungumzia, utagundua, Gavana yupo hapa asubuhi ya leo. Kama una haja, ikiwa uko katika seli ndogo ya maradhi, huwezi kutoka, Gavana yupo hapa. Gavana wa ulimwengu, Yeye ni mwenye haki, na Yeye atakutoa. Yeye alikuja. Akautia sahihi msamaha wako. Yeye anataka tu kukupa huo, asubuhi ya leo. Usiukatae.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

²⁸⁶ Kama unataka ushindi halisi sasa, huku kichwa chako kimeinamishwa, kwa nini usijisalimishe na umwache Gavana wa jimbo, umwache Gavana atie sahihi msamaha wako asubuhi ya leo? Yeye yuko tayari kukutoa; kukutoa kutoka dhambini, kukutoa kutoka katika kutokuamini, kukutoa kutoka katika magonjwa, kukutoa kutoka kwenye chochote unachotaka. Fanya hivyo wakati tukiomba.

Sasa wewe omba kwa njia yako mwenyewe. Zungumza na Yeye. Unaona?

²⁸⁷ Yule askari wa magereza angeweza kuzungumza na gavana. Hilo lisingefaa chochote. Unaona? Ilibidi mvulana huyo kuzungumza na gavana. Unaona?

²⁸⁸ Inakubidi kuzungumza na Gavana. Kama wewe ni mgonjwa, zungumza na Yeye. Kama umetenda dhambi na kufanya makosa, sema na Yeye. Anao msamaha kwa ajili yako.

²⁸⁹ Baba wa Mbinguni, tunashukuru. Nami, Bwana, ni mdeni sana Kwako. Hakuna njia ambayo ningeweza kulipa deni ya dhambi zangu. Nilikuwa kwenye seli siku moja, maana nilizaliwa katika seli hiyo. Nilijua uhuru u—ulimaanisha nini. Nayo gharama ilikuwa ni kubwa mno, nisingeweza kuilipa. Lakini nina furaha sana ya kwamba, ile siku uliyoitembelea seli yangu, nilitambua, ya kwamba Ndiye tu aliyeweza kunisamehe. Jinsi pekee ningaliweza kuwa huru, na kupata ushindi, ushindi mkamilifu, ulikuwa ni kuukubali msamaha ambao Wewe ulikuwa umeutia sahihi kwa ajili yangu. Na leo hii mimi ni huru.

²⁹⁰ Nina furaha sana, Bwana. Mimi hutembelea nyumba moja ya gereza hadi nyumba nyingine ya gereza, kutoka kwa wale walio na matatizo ya ndoa, wale walio wagonjwa na wanaugua, wale walio wagonjwa na katika jela, wale wenye dhambi na katika jela, wale walio na mahangaiko, na mashaka, na katika gereza. Ninaenda kutoka seli moja hadi nyingine, nikiwaambia, Gavana yuaja hivi sasa, akimsamehe kila mmoja, akimtoa kila mmoja nje.

²⁹¹ Baba, unaujua moyo wa watu hawa hapa leo hii. Jalia hii iwe ni siku ya Ushindi, siku ya Ushindi mkamilifu. Jalia hii iwe siku ambapo kila mtu, Bwana, leo hii, atapokea ushindi. Lijalie, Bwana.

²⁹² Jalia kila mgonjwa aponywe, aliye katika jengo hili leo hii.

²⁹³ Jalia upande huu wa nyuma ya jangwa uwe ni wakati ambapo Sauti ya Mungu itazungumza kupitia kwenye—kwenye moto unaowaka wa imani. Ee Mungu, moto huo mdogo unaowaka pale, wa imani, yale matumaini madogo yanayowaka moto, jalia sauti ya Mungu inene kupitia hayo, kwa kila mfungwa asubuhi ya leo, na kusema, “Nimekuja leo kukuweka huru.” Kukiwako na mvulana ama msichana, mwanamume ama mwanamke, hapa, Bwana, asiyejua Wewe kama Mwokozi wao, jalia Sauti hiyo ndogo inene, hiyo imani ndogo, Sauti inayonena sasa na kusema, “Naam, ninaamini ya kwamba Mungu yupo. Ninaamini Yeye ni kila kitu wanachosema Yeye alichu.” Na, Bwana, hebu hiyo imani ndogo iwaweke huru sasa hivi. Tujalie, Bwana.

²⁹⁴ Wabariki. Mbariki Ndugu Isaacson hapa, Bwana. Tunampenda kijana mwanamume huyu na mke wake, watoto wake wadogo. Libariki hili kanisa dogo, Ee Mungu. Kwamba, tuna furaha sana kwa ajili yao, tuna furaha sana kuona ya kwamba wanalo paa juu ya kichwa chao hapa, na mahali hapa ndani. Wewe ni mwema sana kwao, Bwana. Nasi tunakushukuru sana. Jalia sikuzote wadumu wanyenyekevu na wa kupendeza, katika Uwepo wa Mungu.

²⁹⁵ Mbariki mgeni huyu kwenye lango letu. Mbariki mgeni, Bwana. Tunaomba ya kwamba Wewe utakuwa pamoja nao. Na iwapo hawajawahi kupokea ushindi huu mkamilifu, kufikia ambapo wanaweza kusema “amina” kwa kila Neno ambalo Mungu ananena, basi, Bwana, jalia imani yao asubuhi ya leo, waliyo nayo katika Wewe, iitikie kila Neno kwa “amina.” Tujalie, Bwana.

²⁹⁶ Tubariki pamoja. Wakomboe wagonjwa, na wanaoteseka. Jipatie Mwenyewe utukufu.

²⁹⁷ Pia, Mungu mpendwa, jalia tusifadhaike sasa baada ya hili, na tukumbuke ya kwamba majaribu haya na kadhalika yanayotujia, yanafanyika tu kwa sababu Mungu anatupenda. Yeye hutupa sisi, kwa sababu ana imani na sisi. Anaamini ya kwamba tutaninii. . . ya kwamba tunayo imani na upendo kwa ajili Yake, kwamba tutaweza kushinda. Atalihakikisha. Basi jalia tusifadhaike na—na kuingiwa na wasiwasi juu yake. Jalia twende tu kule juu na kunena Neno, na kusonga mbele. Bahari zitafunguka. Siku za Ushindi zitakuja. Tujalie, Bwana. Pia jalia hii iwe moja ya siku za Ushindi zilizo kuu sana za wakati wetu. Tubariki hata tutakapokutana tena, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁹⁸ Ninataka kusema jambo hili, kabla tu haijanibidi kuondoka. Nina saa moja na nusu sasa, kufika Tucson. Ni uendes haji gari si mdogo. Bali ninataka kusema jambo hili, ya kwamba kweli nilifurahia kuwa hapa na kuihisi hii—hii imani mliyo nayo. Kamwe msiiiondokee hiyo. Acheni moto huo mdogo uendelee kuwaka na kuwaka. Pia kumbukeni, Mungu hunena katika mioto hiyo midogo.

²⁹⁹ Ndugu Isaacson, si—sijui tu jinsi ya kulielezea, jinsi nilivyo na shukrani, ya kwamba umeweza kuja huku juu na—na kulishikilia ku—kundi hili pamoja. Mungu, ndugu yangu, na akupe nguvu daima kuendelea. Na kwenu enyi watu mnaokuja kusikiliza, Mungu daima na awape nguvu, nguvu za Kiungu, kuwafanya mwendelee. Sasa kama . . .

³⁰⁰ Ninakisia kidogo mna maagano rasmi katika dakika chache, jinsi, Ndugu Isaacson. Nitamrudishia ibada.

³⁰¹ Na kama kuna yeyote kati yenu hapa, aliye, ambaye amekuwa akisoma kuhusu ubatizo wa maji katika Jina la “Yesu Kristo” badala ya sifa za “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” maskini mchungaji wetu hapa, yupo hapa tayari, atafurahia kufanya hivyo, kufanya ubatizo. Kama kuna matatizo yoyote moyoni mwako, ungetaka aombe kwa dhati pamoja nawe, yeye yupo papa hapa kufanya hivyo. Nami . . . si zaidi ya ninavyomfahamu, na—na kukutana naye, na kuketi pamoja naye, na kadhalika, maskini roho nzuri, nyenyekevu, ya Kikristo inayopatikana ndani ya maskini ndugu huyu. Na—nami nina hakika ya kwamba Mungu huyasikia maombi kama hayo.

³⁰² Ilikuwa kwamba mzee mmoja aliishi nchini mwetu, jina lake Hay. Alikuwa mzee maarufu sana. Alikuwa ni . . . Kila wakati mtu yeyote . . . Alikuwa ni mnyenyekevu na mpole. Lakini, na wengine wao walidhania alikuwa tu ni kichaa wa kidini ama kitu fulani. Lakini, mwajua, wakati mtu yeyote angekuwa mgonjwa, walimwita mzee Daddy Hay aje akawaombe. Hakuwa kichaa hata kidogo wakati huo. Alikuwa ni mtu halisi tu. Basi maskini askari huyo . . .

³⁰³ Kafiri mmoja aliishi huko juu ya kilima pale, alikuwa na shamba. Alikuwa ni rafiki ya baba yangu. Baba yangu alikunywa pombe. Ninaona aibu kusema hilo. Lakini, ukweli ni ukweli, mwajua.

Biblia ni kitu kimoja ambacho husema Ukweli. Mnaona?

³⁰⁴ Sasa, tuna kitabu kinachoitwa historia; kilisema George Washington kamwe hakusema uongo. Ninashuku hilo. Ninashuku hilo. Naam, bwana. Mimi . . . si—si—sininii—siamini hilo. Mtoto anaweza kutokea . . . “Umezaliwa katika dhambi, ukaumbika katika uovu, ukaja ulimwenguni ukisema uongo,” inasema Biblia. Kwa hiyo ni—ninatilia shaka hoja hiyo ya kihistoria ya George Washington. Lakini inasimulia tu sehemu nzuri ya mtu.

³⁰⁵ Biblia husimulia pande zote mbili za mtu. Lutu alikuwa mtu mzuri huko chini Sodoma. “Dhambi za mji ziliitesa nafsi yake yenye haki.” Lakini haikukosa kusimulia kwamba alikaa kinyumba na binti yake mwenyewe na akapata mtoto, hata hivyo, mnaona. Husimulia pande zote mbili zake. Kwa hiyo hatuna budi kusimulia pande zote mbili.

³⁰⁶ Baba yangu, akinywa pombe, aliambatana na kafiri huyu. Naye angemcheka mzee huyu. Daima alikuwa akimdhihakiki. “Mzee Papa Hay,” tulimwita, “Daddy Hay,” maskini mzingo mdogo tu wa nywele. Alikuwa mhubiri mzee. Nao walikuwa wanahitaji mvua wakati mmoja. Mazao yao yote yalikuwa yakiungua. Basi wakaja kwenye kanisa dogo, si zaidi ya hili, lililoitwa Ufalme Mdogo wa Oposamu, huko nyuma Kentucky. Ndipo walipopanda kwenda kule, wanasema yeye alisema . . .

³⁰⁷ Yeye, mzee Daddy Hay, alikuwa na msemu. Yeye angesema, “Kipenzi, naitakia heri nafsi yangu.” Jamaa mdogo, mnyenyekevu, alisafiri na farasi mzee, maskini mhubiri wa kuzungukazunguka. Nao walimlipa labda kwa kikapu kilichojaa maboga yaliyokaushwa, mwajua, na chochote cha ziada walichokuwa nacho, mwajua, na shahamu ama kitu fulani. Hivyo, mwajua, hivyo ndivyo walivyowalipa wahubiri wa kale wa kuzungukazunguka. Wengi wenu ninyi watu hapa mnakumbuka wale wahubiri wa kale wa kuzungukazunguka wa Kimashariki.

³⁰⁸ Basi siku moja mazao yalikuwa yakiungua yote. Naye mzee Daddy Hay akasema, “Vema, kipenzi, naitakia heri nafsi yangu.” Baada ya yeye kufanya ibada ndogo kama hii. Kasema, “Kama yeyote wenu nyote angetaka kubaki na kuomba kwa ajili ya mvua, kwamba Mungu atayanusuru mazao yenu,” akasema, “wewe baki pamoja nami.” Basi kanisa zima likabaki papo hapo pamoja naye.

³⁰⁹ Babangu, huko nje, akaenda kule, jamaa mdogo tu, akatoa matandiko kutoka kwa farasi wake, akayaweka—akayaweka chini ya kanisa, maana alijua ilikuwa inaenda kunyesha.

³¹⁰ Maskini mzee huyo akainama madhabahuni. Hata hakutoka magotini mwake. Kasema, yapata saa moja baada ya hayo, alisikia sauti. Akaangalia kote. Wingu jeusi lilikuwa likija kupitia kilimani. Hiyo hapo. Mnaona?

³¹¹ Yule kafiri, miongoni mwa rafiki za baba waliyemdhihakiki mzee huyo mhubiri, wakati alipokufa, iliwabidi kumshikilia kitandani. Alishikwa na homa ya matumbo ya kutembea. Wengi wenu watu huku nje labda msingejua ilikuwa ni kitu gani. Loo, ni kitu cha kutisha mno. Naye akapigana na pepo saa baada ya saa, kwa muda wa siku tatu ama nne. Angesema, “Charlie, Charlie.” Huyu alikuwa ni baba yangu. Akasema, “Usimwache anipate. Usimwache anipate. Kwani humwoni ameketi pale kando ya kitanda kile pale, amejizungushia hiyo minyororo?

Usimwache anifunge nayo. Loo!” Akapiga makelele. Nao wangemshika, wanaume wanne ama watano wangemshikilia kitandani, kabla hajawa tayari kufa.

³¹² Huko Kentucky, walikuwa na vingingi vya kale kando ya ukuta mahali waliponing'iniza nguo zao. Kuna mtu yeyote aliyepata kuona nyumba kama hiyo, mahali walipobandika kigingi?

³¹³ Naye alikuwa na maskini kotini lake la mvua limewekwa pale juu. Akasema, “Charlie, kuna painti ya wiski mfukoni mwangu. Nenda, ukawapatie watoto wangu.”

³¹⁴ Huku mke wake, Mkristo, yuko huko jikoni, akilia, akipika chakula cha kutwa. Akasema, “Nisingeweza kufanya hivyo.”

³¹⁵ Ndipo wakamshikilia kitandani mpaka akafa, akipigana na pepo wamwondokee.

³¹⁶ Wakati maskini Daddy Hay, yule aliyemcheka, wakati alipokuwa tayari kufa, mwenye umri wa kama miaka themanini na mitano, tisini, alienda kulala. Ndipo watoto wote wakakusanyika humo. Vitukuu vyake wakubwa wakakusanyika kuzunguka kitanda chake. Akainuka. Alikuwa na masharubu meupe, mwajua, mzingo mdogo wa nywele nyeupe kukizunguka kichwa chake. Nini . . . Juu ya kichwa chake, upara. Akapindapinda masharubu yake, kasema, “Kipenzi, naitakia heri nafsi yangu.” Kasema, “Nyote mlidhani mzee Daddy Hay alikuwa amekufa, sivyo?” Akasema, “Vema, siwezi kufa.” Akasema, “Nilikufa miaka mingi iliyopita.” Kasema, “Ninaenda tu kukutana na Bwana Yesu.” Akasema, “Loo, ni kuu sana!” Kasema, “Ninyi nyote, watoto wangu, kusanyikeni kukizunguka kitanda.” Akawashika, kuanzia mwenye umri mkubwa kuliko wote hadi aliye mdogo kuliko wote, kwa mkono, na kuwabariki.

³¹⁷ Ndipo akawaambia wavulana wake wawili wenye umri mkubwa kuliko wote, kasema, “Niinueni juu.” Nao wakamwinua juu kitandani. Asingeweza kuinua mkono wake juu. Alikuwa ni mnyonge sana.

³¹⁸ Akamwambia mvulana wake mwingine, akasema, “Inua mkono wangu juu.” Akainua mikono yake juu, namna *hiyo*.

³¹⁹ Akasema, “Siku yenye furaha, siku yenye furaha, hapo Yesu alipoziosha na kuondoa dhambi zangu. Alinifundisha jinsi ya kukesha na kuomba, na kuishi nikishangilia kila siku.” Akainamisha kichwa chake na akaondoka.

Vema, hatuna budi kufikia mmoja wa miisho hiyo.

³²⁰ Nina furaha kwamba mna maskini mtu mnyenyekevu kama huyu karibu nanyi, mliye na imani naye. Mwaminini; Mungu atafanya miujiza kwa ajili yenu, miongoni mwenu.

³²¹ Nami ninataka kuliomba kanisa hili dogo jambo fulani kwa ajili yangu. Niombeeni, sivyo? Mimi ni mmoja wa ndugu zenu, pia. Siko pamoja nanyi wakati wote; ninataka kuwa.

Mnapata kanda na kadhalika hapa. Nami niko hapa nje kwenye uwanja mkuu wa vita. Hiki ni kimoja tu cha vituo ambako tunakutazamia kule Kuja kwa Bwana. Niombeeni, maana kweli ninahitaji maombi yenu. Ninayategemea, mara nyingi, ninapofikia mahali pagumu, zaidi sana katika maeneo ya ugenini.

³²² Na kuna wachawi, na kila kitu, maelfu mara maelfu wamesimama pale, wakikupa changamoto, nawe unatembea huko nje, peke yako, loo, heri ujue yale unayozungumzia. Loo, jamani! Wakati, wanaweza kufanya lolote. Karibu, wanaweza tu kuiga chochote alichio nacho Mungu. Wanaweza, kama vile tu Yane na Yambre, a-ha, wanaweza kuiga chochote Mungu alichio nacho hapa.

³²³ Ndipo ninakumbuka, ninakumbuka kuhusu kundi dogo, aminifu. “Ni wakati gani, wa siku?” Huko mbali sana upande wa nyuma ya jangwa kule, mbali sana, maskini mahali padogo panapoitwa Sierra Vista, mnaona, mkutano mdogo wa maombi ukiendelea yapata wakati huu. Mnaona? Huko nyuma kabisa, huko ng’ambo ya pili ya mlima, huko juu kwenye maskini ile kambi ya ng’ombe, mahali fulani kama hapo, wanaomba.

³²⁴ Ndipo ninatoka nje, ninasema, “Nimefunikwa kwa maombi. Shetani, huwezi kunifanyia lolote. Ninakuja katika Jina la Bwana Yesu.” Mnaona, jambo fulani linatukia.

³²⁵ Ninyi niombeeni. Mtafanya hivyo sasa, ninyi nyote? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Amina.

Ndugu Isaacson, njoo hapa.

³²⁶ Mwajua, la—laiti ningalikaa huku, na kwenda nyumbani na kila mmoja wenu na kula chakula cha kutwa. Ingenichukua muda mrefu. Nami ninajua nyinyi wanaume mnafikiri mnaye mpishi mzuri kuliko wote duniani. Hapana shaka unaye. Mnaona? Na hakika ningetaka kufanya hivyo. Lakini si—siwezi kulifanya leo. Nyote mnafahamu hilo, sivyo? Ninyi, mnafahamu, kwamba siwezi kufanya hilo sasa hivi. Niko katika mfinyo mkubwa mno hapa, kwenye wakati huu. Ninataka kushuka na kufanya ushirika mdogo pamoja nanyi. Ninataka kurudi tena, pia, kurudi na kuwa pamoja nanyi. Mungu awabariki.

³²⁷ Sasa, Ndugu Isaacson, shika hatamu, lolote Bwana analotaka ufanye.

³²⁸ Sasa, iwapo kuna yeyote wenu ambaye angetaka kuja hapa, ambaye hajawahi kujisalimisha kwa Yesu Kristo, nawe unataka kuja hapa na kusimama hapa asubuhi ya leo, papa hapa karibu na mimbara hii, ambapo mimi na Ndugu Isaacson tumesimama, na unataka kuombewa, unataka tuombe ya kwamba Mungu atakuokoa, hivi utakuja sasa? Na, wewe, utakuwa na ushindi mkamilifu leo hii. Kama utaninii . . .

³²⁹ Iwapo kuna yeyote wenu ambaye amerudi nyuma na kwenda mbali na Mungu, wala hujui—hujui, umepoteza ushirika huo, kama maskini mama yule jana usiku. Loo, giza hukusanyika unapoondoka kwa Mungu. Uko kwenye barabara ya matope. Huna budi kushindwa. Na ikiwa huna ushindi huo unaopaswa kuwa nao, hivi hutakuja, pia? Huu ni ushindi mkamilifu. Hii inaweza ikawa siku ya Ushindi kwa ajili yako, kwa ajili ya mambo yote ya ulimwengu.

³³⁰ Unasema, “Nimekuwa na majaribu mengi sana, Ndugu Branham. Nimekokotwa kabisa huku na huko.” Hivi sijawaambia tu hivi sasa ya kwamba huyo ni Mungu, kwa sababu alikutumaini? Hutampungukia, sivyo? Huenda ulianguka. Huenda ulifanya kosa. Bali hutampungukia, sivyo? Utasimama tena, kama askari halisi, uunyakue Upanga, kisha uje mbele tena. Tungefurahia kufanya hivyo. Hakika.

³³¹ Na kama sivyo, Ndugu Isaacson ataendelea kuwazungumzia basi.

³³² Kama mtaniruhusu sasa, ninaweza kuondoka, kurudi Tucson. Nitarudi kuwaona tena, Bwana akipenda. Mungu awabariki. Mtaniombea sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

³³³ Kumbukeni, mshindi mkamilifu, na uweke fokasi yako kwa Yesu Kristo pekee. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ndipo siku moja, huku jicho lako likitazama mahali pamoja, Yeye atakuja kutoka angani na Mwaliko, Sauti ya Malaika Mkuu. Wafu katika Kristo watafufuka. Nayo miili hii ipatikanayo na mauti itachukua kutokupatikana na mauti, nasi tutaenda kuwa pamoja na Yeye milele. Hadi wakati huo, kesheni mkiomba. Mungu awabariki. 

63-0421 Siku Ya Ushindi
House Meeting
Sierra Vista, Arizona Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org